| ARS-2-15/B | Sokoine | ROYAL ESTATE AGENTS LTD (REA) | ARS-2-BF-11-0-010-1 | R | 911,382.11 |
| ARS-1-566/2/X/E | Kibla | MANGALU FERISTA FLAVIA | ARS-1-BF-66-1-108-1 | R | 1,011,301.20 |
| | | | | | **9,252,213.87** |

## ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA IRINGA

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi ya nyumba | Deni (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| IRA-2-69/II | HAIL | KASANGO EMMANUEL A. | IRA-2-BF-19-0-002-3 | R | 401,634.15 |
| IRA-3-4.090/HKT | IPOG | LUNYUMGU JACSON J. | IRA-3-BF-02-0-075-2 | R | 75,514.00 |
| IRA-3-4.090/HKT | IPOG | MHUFU CHRISTINA | IRA-3-BF-02-0-067-2 | R | 142,056.02 |
| IRA-2-44 I & II/J | MARK | SELEMANI AMER SALIM | IRA-2-BF-09-0-014-1 | R | 464,601.20 |
| IRA-3-4.090/HKT | IPOG | ROBINSON NIKSON | IRA-3-BF-02-0-032-5 | **R** | **213,286.51** |
| IRA-3-4.090/HKT | IPOG | KALIKOWELE ELIZABETH FRANCIS | IRA-3-BF-02-0-072-5 | R | 233,300.27 |
| IRA-2-12/2 | KARM | NDULANGO JOSEPH H | IRA-2-BF-01-0-002-1 | R | 462,293.30 |
| | | | | | **1,992,685.46** |

215678102

Inaendelea ukurasa 7

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tujihadhari corona, lakini tuchape kazi

UGONJWA wa corona, umesambaa kwenye zaidi ya maeneo ya utawala au nchi 187 kati yake 34 ni za Afrika, ikiwa ni watu 294,110 wameambukizwa na kati yake 12,944 wamefariki.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), nchi inayoongoza kwa maambukizi na vifo ni China ikiwa na watu 81,499 huku nje ya China inayoongoza ikiwa ni Italia yenye maambukizi 53,578.

Kila nchi imetangaza hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na ugonjwa huo, huku baadhi zikifunga kila kitu na raia wake hawaruhusiwi kutoka nje na iwapo watakamatwa wanachukuliwa hatua kali. Baadhi zimefungulia wafungwa wote magerezani.

Juzi Rais John Magufuli, alihutubia taifa na kueleza kuwa kuna watu 12 wamegundulika, na hatua zilizochukuliwa ni kwa wote wanaoingia nchini kutoka nchi zenye maambukizi ya corona watawekwa kwenye uangalizi wa siku 14 kwa gharama zao.

Aidha, aliwasihi Watanzania kuendelea na shughuli za uzalishaji, huku wakichukua tahadhari zote muhimu, ikiwa ni siku chache baada ya kutangaza kufunga shule, vyuo na michezo mbalimbali.

Alisema waendelee kuchapa kazi kwa bidii ili kuijenga nchi, na kwamba ugonjwa huo usiwe kigezo au sababu ya kuacha kufanya kazi kwa bidii badala yake iwe hamasa zaidi ya kuchapa kazi.

Tunakubaliana na alichokielekeza Rais kwa kuwa lazima maisha yaendelee, kwa kuwa hata nchi zenye maambukizi ambazo zina uchumi mkubwa kama Italia na Ufaransa shughuli za viwanda zinaendelea kwa tahadhari kubwa, kwa kuwa wanajua wakifunga kila kitu ni sawa na kusimamisha nchi.

Kama nchi kubwa duniani kama hizo zimechukua tahadhari za kuzuia watu kutotoka nje, lakini kazi zinaendelea kwa njia ya mtandao na uzalishaji unafanyika, maana yake ni kuwa licha ya janga lililopo ni lazima uzalishaji uendelee kwa ustawi wa watu wake.

Hivyo, kuendelea na kazi kwa tahadhari kubwa ni suala la kutiliwa maanani, ingawa kwa hali ya umaskini wa nchi zetu, ukosefu wa huduma za mtandaoni ni vigumu sana kwa kazi zote kufanyika kutoka nyumbani.

Wenzetu wameweza kutangaza hivyo kwa kuwa wana uhakika wa miundombinu, watu wake wana utayari wa kufanyakazi na watafanya kwa uaminifu tofauti na nchini ambako mtu anategemea vifaa vya kazi vya ofisi na huduma ya intaneti.

Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania ni wachache wana akiba ya kutosha ya chakula na fedha, wengi ni wale wanaotoka kutafuta mkate wa siku kwamba wakishindwa kutoka basi watashinda njaa. Kwa kuzingatia mazingira hayo, ndiyo maana lazima shughuli za uzalishaji ziendelee, lakini kwa tahadhari kubwa ili maambukizi yasiendelee kusambaa.

Hakuna ubishi kuwa iwapo serikali itatangaza kufunga maeneo yote na watu kuzuiwa kutoka, nchi itasimama. Siyo kila maamuzi yanayofanywa na mataifa mengine kuigwa na nchi yetu, lazima kila uamuzi uzingatie mazingira ya nchi husika.

Sisi tunasema ni vyema kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa fya na kuchukua tahadhari bila kupaniki, huku tukiendelea kutafuta mkate wa siku kama kawaida, na si kukimbilia kufunga biashara au kusimamisha uzalishaji.

Sisi kama taifa, hatuna baba wala mjomba wa kutusaidia bure, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuendelea kufanya kazi za kujenga taifa, huku tukichukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya corona. Mathalani, zipo nchi zimetangaza kusimamisha riba za mikopo, kodi za nyumba na watu wanalipwa mishahara wakiwa nyumbani, kwa serikali yao kutenga fungu la fedha kwa ajili hiyo. Hata hivyo, kwa nchi yetu na nyingine zinazoendelea hali ya uchumi haituruhusu kufanya hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongereni wazazi, walezi kwa uchangiaji huu wa vyakula shuleni

Na Sabato Kasika

ELIMU bora ina faida kwa maisha ya kila mmoja na inachangia ukuaji wa uchumi, na ndiyo maana serikali katika nchi nyingi zinazoendelea na zilizoendelea elimu ni kipaumbele katika mipango ya maendeleo.

Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo, kwani serikali imeipa kipaumbele sekta ya elimu ikiwamo kutoa elimu bure kuanzia elimumsingi hadi kidato cha nne ili kuhakikisha kila mtoto anaelimika.

Pamoja na juhudi hizo, kumekuwapo na changamoto mbalimbali zinazochangia baadhi ya shule kuwa na ufaulu usioridhisha, utoro na mambo mengine yanayokwamisha maendeleo ya watoto shuleni.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wadau wa elimu wamekuwa wakifanya kila njia kuhakikisha wanatoa mchango wa maoni na mawazo yenye lengo la kuinua kiwango cha elimu kwenye maeneo hayo.

Mfano mmojawapo ni , wadau wa elimu wa mkoa wa Mara, ambao mwisoni mwa mwezi uliopita walikutana na kujadili changamoto zinazokwamisha kupanda kwa ufaulu katika shule za msingi na sekondari.

Katika mkutano huo, wadau hao waliibuka na maazimio nane, ambayo wanaamini kwamba ikitekelezwa, itasaidia kupandisha ufaulu na pia kumaliza changamoto nyingine zinazozikabili shule za umma.

Miongoni mwa maazimio hayo ni wazazi kuchangia shuleni kama njia kudhibiti utoro na kuongeza ufaulu, kwa vile mwanafunzi anapokuwa ameshiba anaweza kufuatilia kikamilifu masomo darasani.

Jingine ni kuwapo kwa uhusiano mzuri kati ya walimu na wazazi kama njia mojawapo ya kufuatilia kwa karibu mienendo ya wanafunzi wawapo shuleni na nyumbani ili kama kunakuwapo na tatizo hatua zichukuliwe haraka.

Baada ya maazimio hayo, baadhi ya wazazi wameanza kutekeleza la kuwapo kwa chakula shuleni ili kuhakikisha watoto wao wanakipata wawapo shuleni badala ya kusubiri hadi warudi nyumbani jinoni.

Wazazi hao ni wa Shule za Msingi Chirorwe na Sokoine zilizopo katika kijiji cha Chirorwe, Halmashauri ya Wilaya Musoma, ambao wiki iliyopita walichanga tani 5.6 za mahindi na maharage.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Halamshauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo,wanafunzi wa shule hizo mbili watatumia tani hizo za mahindi na maharage kwa muda wa mwaka mmoja.

Wazazi wamechanga mahindi na maharage kwa kuwa chakula shuleni kinakuza ufaulu wa wanafunzi, kinaboresha afya zao na kupandisha kiwango cha ufaulu.

Tatizo ambalo baadhi ya wazazi wanalo ni kuamini kwamba shule za umma siyo zao na wanadai kwamba serikali ilishatangaza kutoa elimu bure, hivyo hawahusiki kuchangia chakula shuleni!

Kuna haja ya kuwatoa katika mawazo hayo na kutambua kuwa shule za umma ni zao na wao ndiyo umma wenyewe na pia waache kukariri bali watambue wanatakiwa kuzihudumia shule hizo.

Huduma hizo ni pamoja na kuchangia chakula cha wanafunzi ili wapate angalau mlo mmoja wawapo shuleni, kuliko kushinda njaa, hali ambayo inasababisha wasiwe na usikivu wa masomo wawapo madarasani.

Kwa wale wao Mkoa wa Mara, wazazi wa kijiji cha Chirorwe wameonyesha mfano, ambao ni muhimu ukaigwa na wengine mkoani humo ili kuhakikisha kila shule inakuwa na chakula.

Hii inatokana na umuhimu wa chakula, ambao kimsingi ni vigumu wanafunzi kufuatilia masomo kwa umakini iwapo hawajapata chochote kuanzia asubuhi hadi mchana au jioni.

Ninajua wapo baadhi ya watu ambao wamekuwa wakifanya biashara ndogo kama mihogo ya kukaanga kwenye maeneo ya shule, lakini bado haiwezi kumuondolea njaa mwanafunzi.

Vilevile si wanafunzi wote ambao wanapewa pesa na wazazi au walezi kwa ajili ya kununua vitu hivyo shuleni, kwa hiyo jambo la msingi ni wazazi kuchangia chakula shuleni.

Yawezekana vipo baadhi ya vijiji ambavyo vimeanza kutimiza azimio hilo la kuchangia chakula shuleni mkoani Mara, lakini wakazi wa kijiji cha Chirorwe taarifa zao zimewekwa wazi ndiyo maana ninawatolea mfano.

# Benki ya Access yaondoa gharama makato miamala

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Benki ya Access sasa watanufaika baada ya kuondoa gharama ya makato kwenye miamala inayofanyika kwa njia ya simu ukifanya miamala isiyozidi Sh. 200,000 ikiwa ni moja ya njia ya kuwakinga wateja wake na virusi vya corona.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki hiyo jana jijini Dar es Salaam kwa vyombo vya habari, benki hiyo imewahimiza wateja wake na umma kwa ujumla kufanya miamala zaidi kwa kutumia huduma za kibenki kwa njia ya simu inayofahamika kama AccessMobile.

"Mteja ataweza kulipia bili mbalimbali ikiwamo Luku, Maji, Ving'amuzi, kununua muda wa maongezi, kuhamisha pesa kwenda kwenye mitandao ya simu na huduma nyingine.

"Pia tunawahimiza wateja kufanya ununuzi kutoka kwa wafanyabiashara wanaokubali MasterCard QR kwa mfano vituo vya mafuta vya Puma na wafanyabiashara wengine wengi kote nchini, kwani benki yetu ni benki ya kijamii inayowajibika kibiashara kwa biashara ndogo na kubwa chini," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema virusi vya ugonjwa wa corona ni hatari hatua ambayo imeilazimu benki ya Access kuwahamasisha wateja wake kutumia huduma za benki kwa njia ya simu za mkononi ili kuepusha msongamano na safari zisizokuwa za lazima kama ambavyo inashauriwa na wataalamu wa afya.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), hadi jana Machi 23, watu 294,110 walikuwa wameambukizwa virusi hivyo huku 12,944 wakiripotiwa kufariki.

# Milioni 30 wasajiliwa Daftari la Mpigakura

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), imesema jumla ya wapigakura waliopo katika Daftari la Mpigakura awali kwa sasa ni 30,187,987.

Mwenyekiti wa Nec, Jaji wa Rufani mstaafu, Semistocles Kaijage, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa tume na viongozi wa vyama vya siasa.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Kaijage alisema Nec imekamilisha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura awamu ya kwanza.

Alisema uchambuzi unaonyesha, wapigakura wapya walioandikishwa ni 7,043,247 sawa na asilimia 30.41 ya wale wa mwaka 2015 na kwamba idadi hiyo imezidi matarajio na makadirio ya awali kwa asilimia 13.41.

"Idadi ya watu milioni 30.1 inaweza kubadilika baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa uchakataji wa taarifa za wapiga kura endapo watabainika waliojiandikisha zaidi ya mara moja," alisema.

Alisema tume imekamilisha uboreshaji awamu ya kwanza nchi nzima baada ya mchakato kuanza Julai 18, mwaka jana katika mkoa wa Kilimanjaro na Arusha na kukamilika Februari 23, mwaka huu mkoa wa Dar es Salaam.

"Kabla ya kuanza uboreshaji, tume kwa kutumia taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ilifanya makadirio ya wapigakura wapya watakaoandikishwa.

"Makadirio hayo ya uandikishaji yalikuwa ni asilimia 17 ya wapigakura walioandikishwa mwaka 2015 ambao ni 23,161,440."

Kaijage alisema wapigakura waliojitokeza kuboresha taarifa zao ni 3,225,778 sawa na asilimia 13.93 ya walioandikishwa mwaka 2015.

Alisema idadi ya wapigakura 16,707 sawa na asilimia 0.07 ya walioandikishwa mwaka 2015, waliondolewa kwenye daftari kwa sababu wamefariki na wengine kupoteza sifa.

Alisema changamoto walizokutana nazo ni pamoja na kuharibika kwa miundombinu baadhi ya maeneo kutokana na mvua, wananchi kutotumia vizuri siku saba zilizopangwa kwa ajili ya uandikishaji na kusababisha msongamano mwishoni.

"Tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujitokeza kwa wakati kwa muda uliopangwa kwa ajili ya uboreshaji wa daftari awamu ya pili unaotarajia kuanza Aprili 17 na vituo vitafunguliwa kuanzia saa mbili asubuhi na kufungwa saa 12 jioni kwa muda wa siku nne mfululizo," alisema.

Alisema hatua inayofuata ni uwekaji wazi daftari la awali ambao itafanyika kwa mujibu wa vifungu vya 11A na 22 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na kifungu cha 15A cha Sheria ya Uchaguzi Serikali za Mitaa.

Alisema uwekaji wazi wa daftari la awali litawahusu siyo tu wale walioandikishwa awamu ya kwanza bali pia wapigakura wote wa walioandikishwa mwaka 2015.

Kaijage alisema awali tume ilipanga kuliweka wazi daftari hilo pamoja na kuanza uboreshaji awamu ya pili Aprili 26, lakini ilishindwa kwa sababu ya janga la mlipuko wa virusi vya corona.

Pia alisema tume imelazimika kukifuta kikao cha wadau kilichokuwa kifanyike leo kwa kuwa kingehudhuriwa na idadi kubwa ya watu zaidi ya 150.

Viongozi wa vyama vya upinzani walitoa mapendekezo yao kuhusu uboreshaji wa daftari awamu ya pili, ambapo na baadhi walitaka lisifanyike kutokana na janga la corona na wengine wakitaka liendelee.

Mwakilishi kutoka Chama cha Demokrasia Makini, Costa Kibonde, alisema ugonjwa wa corona umeleta shida na wao wamelishuhudia.

"Leo hii tunapata shida, mnaona hata ukaaji wetu kwenye huu mkutano leo tumepeana nafasi moja tunaiacha. Leo ukiingia ofisi za serikali tunanawishwa mikono.

"Leo mnaandaa suala la kuwafanya Watanzania wakusanyike katika vituo, uboreshaji wa daftari awamu ya pili lisitishwe," alisema.

Pamoja na mapendekezo hayo, tume ilisema kuwa imejiandaa na awamu ya pili, na kwamba wanatekeleza hilo kwa mujibu wa sheria kwa sababu hawana mamlaka ya kupelekea muswada bungeni.

Inatoka ukurasa 5



**ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA DODOMA**

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi ya nyumba | Deni (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| DOM-2-17,18,19&20/X | IR | JOSEPH ELIKANA | DOM-2-BF-03-1-102-1 | R | 229,634.59 |
| DOM-2-17,18,19&20/X | IR | BYABATO JOSEPH R | DOM-2-BF-03-2-205-1 | R | 230,300.83 |
| DOM-5-47/00 | MDL | COMPANY ALKAFIL LTD | DOM-5-BF-41-1-103-2 | R | 801,666.67 |
| DOM-5-47/H | MDL | BAGALLA FRANKLIN G. | DOM-5-BF-2-0-002-2 | R | 874,301.77 |
| DOM-4-1/F-B | MPWN | KANGOZI MICHAEL JUDITH | DOM-4-BF-09-0-004-3 | R | 632,079.87 |
| DOM-5-480-491,493-525/00 | KONG | MWAKIBIBI MARTHA J | DOM-5-SM-034-0-002-1 | R | 291,001.92 |
| DOM-4-1/F-B | MPWN | PAUL JAMES NGWEGWE | DOM-4-BF-09-0-004-5 | R | 753,129.34 |
| DOM-4-1/F-B | MPWN | MWAGAYAGILE BLESSED | DOM-4-BF-09-0-006-2 | R | 880,342.12 |
| DOM-5-480-491,493-525/00 | KONG | MBWANA JOBA | DOM-5-SM-15-0-032-1 | R | 402,506.95 |
| DOM-4-2/F | MPWO | MKANDE CHRISTOPHER | DOM-4-BF-10-2-205-1 | R | 511,294.01 |
| | | | | | **5,606,258.07** |

**ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA KIGOMA**

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi | Deni (Tsh) ya nyumba |
|---|---|---|---|---|---|
| KGM-1-210/00 | MNG | M/S MAJARIBU TRADING CO LTD NIL | KGM-1-BF-009-0-006-3 | R | 399,551.50 |
| | | | | | **399,551.50** |

**ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA LINDI**

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi ya nyumba | Deni (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| LND-1-11/A | UHR/KRM | CHILIPWELI SILA JOHN | LND-1-BF-018-1-101-2 | R | 442,520.60 |
| LND-1-15/B | AZM/AMN | MWIDADI YUSUFU AMANI | LND-1-BG-012-0-001-4 | R | 631,820.94 |
| LND-1-16/B | AM | KALADUSHI SOSTENENS GOBANYA | LND-1-BG-013-0-002-4 | R | 398,505.67 |
| LND-1-11/B | AM | MAGHEMBE V.M | LND-1-BF-016-2-201-3 | R · | 1,796,916.04 |
| LND-1-24 & 26/B | AZM/KRM | MKUCHU DENNY | LND-1-BF-011-1-102-1 | R | 539,968.60 |
| LND-3-5-6/Z | WLS | MTOPA ALLY MOHAMED | LND-3-BG-038-0-001-2 | R | 727,438.50 |
| LND-1-24 & 26/B | AZM/KRM | TCCIA MKOA | LND-1-BF-011-1-1 | R | 298,552.15 |
| LND-1-17/B | BRZ | MEIS INDUSTRY COMPANY MIC | LND-1-BF-014-0-007-1 | R | 6,499,592.55 |
| LND-1-24 & 26/B | AZM/KRM | JAFFER ANWAR MOHAMED | LND-1-BF-011-0-004-3 | R | 306,581.67 |
| LND-1-23 & 25/B | KRM/ELT | TCCIA (M) LTD TCCIA | LND-1-BF-010-0-005-3 | R | 2,894,285.35 |
| LND-1-9/B | KRM/AMN | BAMINGO COMPANY B | LND-1-BF-015-0-005-2 | R | 356,383.50 |
| | | | | | **14,892,565.57** |

**ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA KILIMANJARO**

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi ya nyumba | Deni (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| MSH-4-I-XBLC/URU | URU ROAD | CHIKIRA ABRAHAM | MSH-4-BF-003-1-104-1 | R | 183,503.09 |
| MSH-3-4/A | BOMA | MSANGI HAWA HASSAN | MSH-3-BF-002-1-103-2 | R | 621,054.94 |
| MSH-2-24/00 | OLD MOSHI | NGELULA LEONARD | MSH-2-BF-032-1-111-2 | R | 73,470.13 |
| MSH-4-I-XBLC/URU | URU ROAD | MWAKALINGA MARTIN | MSH-4-BF-007-0-004-1 | R | 187,302.60 |
| MSH-2-24/00 | OLD MOSHI | RUGAKINGIRA PHILBERT CHRISTIAN | MSH-2-BF-032-0-019-5 | R | 899,862.75 |
| MSH-3-83/B | RINDILANE | J.S. KHAMBAITA LIMITED | MSH-3-BF-027-0-002-2 | R | 674,880.00 |
| MSH-3-39/B | KIBO/REN | BENANDYS LTD LTD | MSH-3-BF-001-1-101-2 | R | 4,456,895.18 |
| MSH-2-27/00 | OLD MOSHI | TILYA NICHOLAUS A. | MSH-2-BF-034-0-002-2 | R | 1,450,702.83 |
| MSH-3-22/B | RENGUA | ASSENGA SYLVESTER P. | MSH-3-BF-015-0-003-5 | R | 2,007,885.80 |
| MSH-3-4/B | BOMA | LABOPHARMA LTD MAULIDI MARIWA | MSH-3-BF-013-0-017-1 | R | 1,705,044.20 |
| MSH-3-3/B | BOMA | TANSCAN TIMBER LTD. | msh-3-bf-012-0-003-1 | R | 3,713,126.35 |
| | | | | | **15,973,727.88** |

**ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA MOROGORO**

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi ya nyumba | Deni (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| MGR-3-96/1/II | OLD DSM RD | KIYAME BEATRICE BLANDISH | MGR-3-BF-039-2-206-4 | R | 282,000.23 |
| MGR-3-15/II | STATION RD | MSOMALI HALIMA MOHAMED | MGR-3-BF-047-1-102-2 | R | 903,507.14 |
| MGR-2-32/B | BOMA RD | MASAKI ROBISON A. | MGR-2-BF-027-0-003-3 | R | 983,085.59 |
| | | | | | **2,168,592.96** |

**ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA MARA**

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi ya nyumba | Deni (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| MUS-2-12-16/E | MK | M/S UBAPA COMPANY LIMITED | MUS-2-BF-30-1-117-2 | R | 1,117,722.87 |
| | | | | | **1,117,722.87** |

**ORODHA YA WAPANGAJI WANAODAIWA WALIOHAMA NA KUACHA MADENI - MKOA WA TANGA**

| Kiwanja Namba | Mtaa | Jina la Mpangaji | Akaunti Namba | Matumizi ya nyumba | Age | Deni (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| TAN-2-12/KBV | EUCKEN | MANAGING DIRECTOR ECKENFORDE EDUCATION INSTITUTE LTD | TAN-2-BF-21-0-3 | R | 4.87 | 15,401,933.19 |
| | | | | | | **15,401,933.19** |

**WAPANGAJI WALIOHAMA NA KUACHA MADENI KWENYE MIKOA YA NHC**

| SNA | MKOA | JUMLA YA MADENI |
|---|---|---|
| 1 | ARUSHA | 9,253,231.87 |
| 2 | DODOMA | 5,606,258.07 |
| 3 | ILALA | 964,179,125.30 |
| 4 | IRINGA | 1,992,685.46 |
| 5 | KIGOMA | 399,551.50 |
| 6 | KILIMANJARO | 15,973,727.88 |
| 7 | KINONDONI | 115,462,015.65 |
| 8 | LINDI | 14,892,565.57 |
| 9 | MARA | 1,117,722.87 |
| 10 | MBEYA | 15,979,233.32 |
| 11 | MOROGORO | 2,168,592.96 |
| 12 | MTWARA | 4,086,269.75 |
| 13 | TANGA | 15,401,933.19 |
| 14 | TEMEKE | 232,928,281.59 |
| | | **1,399,441,194.97** |

**IMETOLEWA NA:**
**KITENGO CHA MAWASILIANO KWA UMMA NA HUDUMA KWA JAMII**
**NHC MAKAO MAKUU**

215678102

# Chadema yampoteza Makongoro Mahanga

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimepata pigo baada ya kada wake na aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Ilala, Dk. Makongoro Mahanga, kufariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, jijini Dar es Salaam jana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii iliyosainiwa na Ofisa habari wa chama hicho Kanda ya Pwani, Lyenda Gervas, kiongozi huyo alifariki saa 12:30 asubuhi katika hospitali hiyo alikokuwa amelazwa tangu Machi 21, mwaka huu.

"Dk. Mahanga amefikwa na mauti akiwa anapata matibabu kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Dk. Mahanga aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana katika Serikali ya awamu ya nne na baadae mwaka 2015, alihamia Chadema.

Aliwahi kuwa mbunge kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi katika Jimbo la Ukonga jijini Dar es Salaam kwa miaka 10 mfululizo kuanzia mwaka 2000 mpaka 2010, kabla ya jimbo hilo kugawanywa na kupatikana Jimbo la Segerea alikoshika nafasi hiyo kwa miaka mitano.

Mwaka 2015, Dk. Mahanga aligombea tena ubunge kwenye jimbo la Segerea kwa tiketi ya Chadema, lakini aliangushwa na mgombea wa CCM, Bonnah Kamoli, anayeshikilia kiti hicho hadi sasa.

Dk. Mahanga ndiye pekee aliyebaki Chadema miongoni mwa waliokuwa makada wa CCM waliohamia upinzani wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, wengine walikuwa ni mawaziri wakuu wastaafu Edward Lowasa na Fredrick Sumaye.

Pia, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Juma Mwapachu na aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Ardhi ,Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Goodluck Ole Medeye ambao wote kwa sasa wamerejea CCM.

Baada ya kuhamia upinzani, Mahanga alikuwa mmoja wa wakosoaji wakubwa wa serikali na kuonekana kuwa mtu muhimu katika upinzani, hata hivyo kada huyo alipowania uongozi wa ndani ya chama katika nafasi ya Katibu wa Baraza la Wazee Chadema (Bazecha) alishindwa na mpinzani wake na Katibu wa sasa wa baraza hilo, Rodrick Lutembeka.

Wakati huo huo, Chama cha ACT-wazalendo kimetoa pole kwa Chadema kufuatia kifo cha kada wake, katika taarifa iliyotolewa na Naibu Katibu wa Idara ya Habari, Uenezi na Mahusiano kwa Umma, Janeth Rithe, chama hicho kimetoa pole kwa familia na chama kwa ujumla.




Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. Kushoto ni Mwenyekiti wa Kanda ya Kati wa chama hicho, Lazaro Nyalandu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

**TAARIFA KWA UMMA**

***19 Machi,2020***

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inawatangazia wadau wake wote na umma kwa ujumla kuwa, pale **pasipo na ulazima wa kufika katika Ofisi za EWURA,** watumie mawasiliano ya simu na mtandao kupata huduma.

Hatua hii inachukuliwa ili kuendelea kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).

Wadau wanashauriwa kutumia mawasiliano yafuatayo:-

**Simu: (1) 0800110030 (BURE)**
**(2) +255-26 2329002-3**

**Barua pepe: info@ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU**

21567402

# Rada mpya kufungwa katika mikoa mitatu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amesema katika kuboresha huduma za hali ya hewa nchini, serikali imenunua rada tatu ambazo zitafungwa katika mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Hali Hewa Duniani yaliyofanyika katika Ofisi za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Kamwelwe, alisema baada ya kufungwa rada hizo kutakuwa na mtandao wenye rada tano, ambazo zitakuwa na uwezo wa kuliona anga la Tanzania kwa asilimia 70.

Alisema kutokana na uwekezaji wa serikali katika sekta ya hali ya hewa nchini, huduma zinazotolewa na mamlaka hiyo kwa sasa zimeendelea kuongeza viwango vya ubora pamoja na usahihi wa utabiri.

Waziri huyo alisema kwa sasa usahihi wa utabiri wa hali ya hewa upo kati ya asilimia 88 na 96, viwango ambavyo ni juu ya viwango vinavyokubalika ambapo viwango vya kimataifa ni asilimia 70.

"Haya ni mafanikio makubwa katika kutekeleza sera na mikakati ya serikali ya awamu ya tano sambamba na kutekeleza mkataba wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), hivyo natoa wito kwa wadau wote wa hali ya hewa kushiriki shughuli za maendeleo za sekta hii," alisema Kamwelwe.

Aidha, Waziri Kamwelwe alisema, uboreshaji wa huduma hiyo utasaidia kukabiliana na majanga mbalimbali, yakiwamo mafuriko na vimbunga.

"Taarifa za hali mbaya ya hewa zinapotolewa kwa wakati huwezesha serikali kukabiliana na majanga hayo," alisema.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kuboresha mtandao wa vituo vya ufuatiliaji na upimaji wa hali ya hewa nchini, utabiri wa hali ya hewa kwa ajili ya matumizi ya maamuzi katika sekta mbalimbali ikiwamo ya maji, kilimo na uchukuzi ili kuhakikisha serikali na wananchi wanapata taarifa sahihi.

Kadhalika, Kamwelwe alisema miongoni mwa mambo muhimu ambayo serikali imetekeleza katika kuboresha huduma ya sekta hiyo ni pamoja na kutunga Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Namba 2 ya Mwaka 2019.

"Sheria hii inaiwezesha TMA kutekeleza majukumu yake kitaifa, kikanda na kimataifa katika kutoa huduma kwa ubora na ufanisi zaidi. Aidha, sheria hii inaipa TMA nguvu ya kudhibiti huduma za hali ya hewa zinazotumiwa kibiashara," alisema.

**Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kuboresha mtandao wa vituo vya ufuatiliaji na upimaji wa hali ya hewa nchini, utabiri wa hali ya hewa kwa ajili ya matumizi ya maamuzi katika sekta mbalimbali ikiwamo ya maji, kilimo na uchukuzi ili kuhakikisha serikali na wananchi wanapata taarifa sahihi.**

HABARI KITAIFA

# DC awaonya wanaosambaza mzaha mitandao kijamii

**Na Manuel Kaminyoge, SONGWE**

MKUU wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo, amewaonya watu wanaotumia mitandao ya kijamii kutengeneza na kusambaza mizaha na taarifa za uongo kuhusu ugonjwa wa virusi vya corona kuwa watachukuliwa hatua kali.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Songwe katika kikao cha kutathmini utayari wa kupambana na ugonjwa huo mkoani hapo, alisema mizaha ya kwamba ugonjwa huo hauwapati watu weusi inadhoofisha mapambano na kuwafanya wananchi wengine kutotilia maanani maelekezo ya wataalamu wa afya ya tahadhari.

Alisema licha ya Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA) kutangaza kuwachukulia hatua kali wote wanaosambaza mizaha na taarifa za uongo, uongozi wa Mkoa wa Songwe na wilaya zote hautawavumilia watakaofanya vitendo hivyo mkoani hapo.

Aliwataka wazazi na walezi wote kuangalia watoto wao wasizagae mitaani, sokoni, minadani na katika mikusanyiko ya masomo ya ziada (tuisheni) kwa kuwa serikali imefunga shule ili kuchukua tahadhari ya kuwakinga wanafunzi.

Alisema serikali inaendelea kusisitiza sehemu ambazo lazima mikusanyiko iwepo kama katika nyumba za ibada na katika ofisi mbalimbali, maji ya kunawa na sabuni yawepo na pia hatua zote muhimu za tahadhari zichukuliwe.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Songwe kuacha masuala ya mila yanayoweza kuwaweka katika hatari ya kuambukizana virusi hususani utamaduni wa kusalimiana kwa kushikana mikono.

Pia, alisema wananchi wasisubiri ifikie hatua ya kutibu wagonjwa bali wazuie kwanza kwa kuchukua tahadhari ya kujikinga kwa kuwa ikifikia hatua ya kutibu watu wengi wanaweza kupoteza maisha.

"Serikali ya Mkoa wa Songwe na wilaya zake haitacheka na mtu yeyote atakayebainika kuleta mzaha kwenye suala la corona, ole wake," alionya Palingo. Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Hamadi Nyembea, alisema Mkoa wa Songwe unatoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo kwa wananchi kwa ngazi zote.

Alisema kamati za afya za wilaya hadi ngazi ya kata zitahakikisha zinafikisha elimu ya kujikinga.

Sauli Ndambo, mkazi wa Ilembo, Wilaya ya Mbozi aliishukuru serikali kwa kuchukua tahadhari na kufunga shule ili watoto wawe salama huku akiwataka wanaofanya mizaha kuacha mara moja kwa kuwa ugonjwa huo hauna mzaha na unaua.



Kijana akibebeshwa gunia la maparachichi, ili kujipatia kipato cha siku katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi yanasa mbao 390 kwa madai kusafirishwa bila kibali

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, limekamata mbao 390 ambazo zilikuwa zinataka kusafirishwa kupelekwa Kisiwa cha Unguja bila ya kibali.

Akizungumza na Nipashe wilayani Wete, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alieleza kuwa mbao hizo zilikuwa zimeshapakiwa katika gari la kampuni ya Seastar 1 kwa ajili ya kusafirishwa.

Alieleza kuwa tukio hilo lilitokea saa 6:30 usiku katika Kijiji cha Kiungoni Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kamanda Sadi alieleza kuwa katika harakati hizo walimkamata dereva wa gari hilo pamoja na wakala wa mzigo huo, lakini mwenye mali hakupatikana kwa muda huo.

"Tulifanikiwa kukamata gari moja ambalo lilikuwa limepakia mbao 390 ambazo zilikuwa zinataka kusafirishwa kwenda Unguja," alisema Kamanda Sadi.

Alisema wakala wa mbao hizo ambaye alitambulika kwa jina la Salum Mohammed Seif na saa 7:00 ndio walifanikiwa kumkamata mwenye mzigo huo, Omar Ali Omar.

Kamanda Sadi alifafanua kuwa mbao hizo zilikuwa zinataka kusafirishwa bila ya kuwa na hati ya kusafirishiwa licha ya kuwa na kibali cha kukatia mti.

"Wito wangu kwa jamii tufuate sheria ili tuweze kuepukana na matatizo yasiyo ya lazima, mwananchi yeyote ambaye anataka kusafirisha mzingo ni lazima awe na cheti maalum cha kusafirishia," alisema Sadi.

Naye Kaimu Ofisa Idara ya Misitu na Mali Zisizorejesheka Pemba, Mussa Said, alieleza kuwa baada ya watuhumiwa hao kukiri kosa lao hilo, Polisi walikabidhiwa ili taratibu za kisheria zichukuliwe.

"Baada ya kuchukuliwa maelezo kituo cha Polisi na kukubali kosa lao, watuhumiwa hawa tulikabidhiwa sisi ili tuweze kuchukua hatua stahiki dhidi yao... tumewatoza faini Sh. 700,000," alisema Mussa.

Mussa alitoa wito kwa wananchi wanapotaka kusafirisha mizigo yao ni lazima wawe na kibali maalum cha kusafirishia mizigo yao.

# Kahama waomba elimu zaidi tahadhari kwa vijana

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

BAADHI ya wananchi wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wameiomba serikali kuendelea kutoa elimu ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID -19) ili kila mwananchi achukue tahadhari.

Wito huo ulitolewa jana na wananchi hao wakati wakizungumza na Nipashe kufuatia uwapo wa ugonjwa wa corona katika mataifa mbalimbali duniani na kuwa bado jamii inaona ugonjwa huo ni mzaha.

Jasmin Athumani, mkazi wa Nyakato mjini Kahama, alisema kundi kubwa ambalo bado linaleta mzaha ni la vijana hivyo ni lazima serikali ielekeze nguvu kwa ajili ya kuwapa elimu ili watambue kuwa ugonjwa huo ni janga la kitaifa na kuwachukulia hatua wenye kuleta mzaha.

Lucas Kulwa, mkazi wa Kagongwa na Sabato Mwita, mkazi wa Majengo walisema wanaipongeza serikali kwa juhudi inazoendelea kuchukua dhidi ya ugonjwa wa corona na kuomba kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari na matangazo mbalimbali ili kila mmoja afahamu kuwa ugonjwa huo ni tishio duniani.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. Lucas David, alisema halmashauri hiyo imejipanga kukabiliana na ugonjwa huo na kuwapongeza wananchi kwa ushirikiano wanaoutoa kwa mamlaka husika kukabiliana na ugonjwa huo na kwamba hakuna mgonjwa aliyebainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa corona katika halmashauri hiyo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliwataka wananchi kutokuwa na taharuki yoyote kuhusu ugonjwa huo badala yake waendelee kuchukua tahadhari na usiwe chanzo cha watu kutofanya kazi za kujiimarisha kiuchumi.

Jumapili iliyopita Rais John Magufuli akizungumza na taifa katika Ikulu ndogo ya Chamwino, jijini Dodoma alisema Tanzania imebaini wagonjwa 12 hadi Jumapili na kuanzia jana wasafiri watakaoingia nchini kutoka nchi zenye maambukizi ya corona watawekwa katika eneo maalum kwa siku 14 kwa gharama zao wenyewe.

**Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. Lucas David, alisema halmashauri hiyo imejipanga kukabiliana na ugonjwa huo na kuwapongeza wananchi kwa ushirikiano wanaoutoa kwa mamlaka husika kukabiliana na ugonjwa huo na kwamba hakuna mgonjwa aliyebainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa corona katika halmashauri hiyo.**

HABARI KITAIFA

## Watendaji watakiwa kuibua wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WATENDAJI wa Idara ya Watu Wenye Ulemavu Visiwani Pemba, wametakiwa kuendelea na juhudi za kuwafichua na kuwasaidia watu wenye ulemavu, ili kupata haki zao za msingi, ikiwamo elimu.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Panya Ali Abdallah, kamati hiyo ilipowatembelea familia za watu wanaoishi na ulemavu Mfikiwa na Wesha Wilaya ya Chakechake Pemba.

Alisema ni jambo la faraja kuona serikali inachukua jitihada za kuwafichua watu wanaoishi na ulemavu, hivyo msichoke kuwatafuta na wengine, ili waweze kupata haki zao za msingi ikiwamo elimu na mahitaji mengine.

"Tunashukuru sana kutumia nguvu za ziada kuwaelimisha wazazi katika familia hii ya Mfikiwa mpaka wakakubali kumpeleka mtoto wao shule, hivyo tuwatafute wengine tuwasaidie, kwani naweza kufanya mambo makubwa na ya kuishangaza jamii," alisema mwenyekiti huyo.

Aidha, aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi wanazozichukua kwa kusaidia wananchi kupitia miradi ya kaya maskini inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ambapo awamu ya tatu italenga watu wenye mahitaji maalumu.

"Ni jambo la faraja kuona kuwa awamu ya tatu ya Tasaf inakuja kulenga watu wenye mahitaji maalumu, hivyo tuwafichue ili utakapokuja huu mpango wapate kusaidiwa," alisema.

Mwenyekiti huyo pia aliwataka wazazi kutowaficha watoto wenye ulemavu na badala yake waunge mkono juhudi za serikali za kuwaangalia wenye hali ngumu na wenye mahitaji maalum na kuwasaidia.

Wakati huo huo, kamati hiyo ilitembelea jumuiya ya kuelimisha athari za dawa za kulevya na mimba katika umri mdogo (JUKAMKUM), ambapo mwenyekiti huyo aliitaka jumuiya hiyo wanapoandaa takwimu zao ziwe na usahihi, kwani ni muhimu na itakuwa imeisaidia serikali.

Mratibu wa JUKAMKUM, Sifuni Ali Haji, alisema kuwa wamekuwa wakitoa elimu ya homa ya ini, kifua kikuu, maradhi ya kujamiiana, afya ya uzazi, kugawa kondomu, kutoa vipeperushi na ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa vijana.

"Kwa kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2019 tumeshawafikia vijana 1,068 kwenye vijiwe na vyuo vya mafunzo, lakini tunakabiliwa na changamoto ya vitendea kazi, pamoja na ofisi ya kudumu, licha ya kazi kubwa wanayoifanya," alisema.

# Zungu aanika faida za mabasi ya mwendokasi kudhibiti hewa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amesema miradi ya reli ya kisasa (SGR) na Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ni jitihada za serikali katika kupambana na athari za hewa ya ukaa.

Zungu aliyasema hayo alipotembelea Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji Hewa ya Ukaa (NCMC) kilichoko katika Chuo cha Kilimo (SUA) mjini Morogoro, akikipongeza kwa utendaji mzuri na kuahidi kuzifanyia kazi matatizo yanayokikabili.

Alisema pamoja na jitihada za serikali kupambana na hewa ya ukaa, kuna haja wananchi kutumia nishati mbadala, kupanda miti ambayo kwa namna moja inasaidia katika kupunguza hewa ya ukaa.

Alitahadharisha kuwa hewa ya ukaa inaweza kuwa na athari kubwa kwa vizazi vijavyo kama jamii haitaamua kuchukua hatua katika kupambana na tatizo hilo.

Alipongeza jitihada zinazofanywa na serikali na kutoa wito kwa wananchi ambao ni wadau wakubwa wa mazingira, kutoa mchango wao na kushirikiana na serikali katika kukabiliana na hewa ukaa.

"Tunataka sasa wananchi wajue madhara ya kulima kwenye vyanzo vya maji na athari ya hewa ukaa inatokana na shughuli za kibinadamu hasa ukataji wa miti na tumesikia taarifa hapa ya namna miti inavyopotea kuanzia mwaka 2002 hadi mwaka 2013, miti takriban 464,000 imepotea, hii ni hatari kwani inaweza kusababisha nchi kuelekea kuwa jangwa," alionya.

Aliipongeza NCMC kwa kazi nzuri wanayofanya na kuiomba kukamilisha taratibu ili kupata fedha kutoka Hazina ambazo zitasaidia kukifanya kituo kiwe chini ya SUA badala ya kutegemea wafadhili kutoka nje.

Awali akiwasilisha mada, Mratibu wa Kituo hicho, Profesa Eliakimu Zabibu, alisema Tanzania ambayo ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), itafaidika na sera kama Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa kutokana na ukataji miti ovyo na uharibifu wa Misitu (MKUHUMI (REDD+).

Profesa Zabibu alisema faida za Mkuhumi ni kuimarisha utunzaji misitu nchini na kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

Alisema ili nchi ishiriki katika shughuli za Mkuhumi, ni sharti ikamilishe vigezo vya kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Upunguzaji wa Hewa Ukaa pamoja na mpango kazi, kuandaa takwimu za msingi za kiwango rejea cha hewa ukaa kinachozalishwa kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu nchini (Forest Reference Emission Level-FREL).

Pia ni lazima kuanzisha mfumo madhubuti wa upimaji, uwasilishaji na uhakiki wa kaboni, kuweka mfumo wa kinga za athari zinazoweza kutokea kutokana na utekelezaji wa shughuli za Mkuhumi (REDD+Safeguard System) na kuandaa mfumo wa wazi na thabiti wa malipo yatokanayo na utekelezaji wa Mkuhumi.



Wachuuzi wa samaki wakisafisha kitoweo hicho baharini, baada ya kuwapaa na kuwaondoa magamba katika soko la Feri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Takukuru yarejesha fedha za wanakijiji

**Na Ashton Balaigwa, KILOSA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Morogoro, imefanikiwa kurejesha Sh. milioni 2.3 kwa wananchi 15 ambao walichangishwa kwa njia ya utapeli na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mlimani Boma, Kata ya Kasiki wilayani Kilosa kwa ahadi ya kupimiwa viwanja vya makazi eneo la Mlimani Boma.

Akizungumza kwenye kikao cha kukabidhi fedha kwa wananchi hao wilayani Kilosa, Mkuu wa Takukuru Mkoa Morogoro, Janeth Machulya, alisema katika uchunguzi wao walibaini kati ya Desemba mwaka jana na Januari mwaka huu, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Hosea Mgunda, alipokea jumla ya Sh. milioni 2.36 kutoka kwa wananchi, akiwaahidi kuwapimia viwanja vya makazi katika eneo la Mlimani Boma.

Alisema uchunguzi wao pia ulibaini kuwa eneo hilo ni la umma na limehifadhiwa na serikali kwa matumizi ya shughuli za umma, lakini kiongozi huyo wa bila kujali dhamana aliyopewa, alifanya dhuluma hiyo kwa wananchi anaowasimamia.

Machulya alisema wakati wa uchunguzi, mwenyekiti huyo alikiri kuchukua fedha hizo kutoka kwa wananchi hao kisha kuwaaminisha kuwa atawapimia viwanja, huku akijua kuwa eneo hilo ni kwa ajili ya matumizi ya umma.

"Sisi, Takukuru tulimwagiza kurudisha fedha hizo haraka. Pamoja na agizo hilo, hatua kali za kinidhamu zitaendelea kuchukuliwa dhidi yake," alisema.

Kiongozi huyo wa Takukuru alisema kwa kutambua jitihada kubwa zinazoendelea kufanywa na serikali ya mkoani humo katika kupambana na tatizo la migogoro ya ardhi, Takukuru itazidi kuchukua hatua dhidi ya baadhi ya watendaji wa serikali za mitaa wasio waadilifu.

"Sisi tutaendelea kuwachukulia hatua kwa kuwa imefikia hatua baadhi ya watendaji hao kujitwalia maeneo ya umma na kuyauza kama mali yao binafsi au kupokea fedha kwa ahadi kuwa watawapatia maeneo hayo wananchi wanaohitaji huku wakijua kuwa ni kinyume cha sheria na taratibu za nchi," alionya.

Alisema Takukuru haitasita kumchukulia hatua za kisheria mtendaji yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo ili watambue dhamana kubwa waliopewa kwa wananchi wanyonge ambao serikali imekusudia kuwalinda.

Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Mgunda, akizungumza kwenye kikao cha pamoja na viongozi wa serikali ya Wilaya ya Kilosa chini ya Mkuu wa Wilaya hiyo, alikiri kukusanya fedha kutoka kwa baadhi ya wananchi.

Hata hivyo, alidai kuwa hakufanya hivyo kwa ajili ya kuwapatia viwanja, bali kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mwenyekiti wa Kitongoji na hakuwa na lengo baya la kujinufaisha.

# DC ashauri wazazi kufuatilia watoto

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewaasa wazazi kutumia muda wao mwingi kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, badala ya kutumia muda mwingi kuchati kwenye simu za viganjani.

Aliyasema hayo jana wilayani humo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na malezi ya wazazi kwa watoto wao.

Muro alisema kuwa, wazazi wengi wanatumia muda mwingi kwenye simu za kiganjani na kusahau majukumu ya kuwalea watoto wao, hali inayochangia kuharibika kwa watoto wao na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

"Unajua wazazi wa siku hizi wanapoteza muda mwingi kwenye simu za mkononi, kuliko watoto wao unakuta mzazi anachati muda wote badala ya kukaa na watoto wao na kukagua madaftari, ili kujua maendeleo ya masomo yao na kuwatia moyo," alisema na kuongeza:

"Mwisho wa siku inachangia kupata matokeo mabaya katika masomo yao. Wazazi nawaombeni sana mjitahidi kuwa karibu kufuatilia maendeleo ya watoto wenu shuleni, kwani tunapowaacha watoto bila kuwaangalia.

"Mwisho wa siku wanaishia kuwa makahaba na wavuta bangi na watakaoteseka ni sisi wenyewe wazazi, hivyo ni vizuri mkawaandaa watoto wetu vizuri ili kuepuka mambo hayo."

Muro alisema watoto hujengwa tangu wakiwa wadogo kwa kufuatiliwa kila wanachofanya, hivyo anapoachwa huishia kuharibikiwa na mwisho siku anayepata hasara mzazi.

Alisema ni vema kila mzazi akabadilika na kuachana na simu ambazo zinachukua muda mwingi, badala yake muda huo watumie kwa watoto wao.

# Mviwata yaiangukia serikali viuatilifu

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MTANDAO wa Vikundi vya Wakulima nchini (Mviwata), umeiomba serikali kuingilia kati na kudhibiti uingizwaji holela wa viuatilifu nchini ili kumaliza changamoto ya viuatilifu feki na visivyo na viwango.

Viuatilifu hivyo feki na visivyo na viwango vinashindwa kuua wadudu waharibifu wa mimea.

Kauli hiyo ilitolewa juzi jijini hapa na Mwenyekiti wa Mviwata, Mkoa wa Arusha, Mchungaji John Safari, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusiana na changamoto ya mazao ya wakulima kuvamia na wadudu.

Alisema kuwa wakulima wengi nchini wamekumbwa na adha kubwa ya mazao yao kushambuliwa na wadudu kiasi cha kukosa mavuno, kutokana na dawa zinazoingizwa nchini kutokuwa na uwezo wa kuua wadudu waharibifu.

"Hivyo tunaiomba serikali kupeleka wataalamu wa kilimo vijijini ili kufanya utafiti wa baadhi ya wadudu wasiosikia dawa na kupata dawa zenye uwezo wa kuuangamiza, lakini watusaidie kudhibiti viuatilifu feki vinavyoingia kinyemela nchini," alisema.

Alisema changamoto kubwa kwa wakulima jinsi ya kupata dawa za kuua wadudu kwenye mazao yao kwani kwa sasa wadudu wamekuwa sugu, hawasikii dawa na kujikuta wakipata hasara kila mwaka.

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema serikali imejipanga kutatua changamoto zote zinazowakabili wakulima, hususani wanachama wa Mviwata ili kuboresha shughuli zao za kilimo.

"Lakini sio kujipanga tu bali hata suala la upatikanaji wa mbolea na pembejeo zingine nalo serikali tunalipa kipaumbele, hivyo msiwe na shaka na serikali yenu," alisema.

Akizungumzia suala la viuatilifu alisema kumekuwapo na tatizo la uelewa juu ya matumizi ya viuatilifu kwa wakulima, hivyo kuchangia sehemu kubwa ya wadudu kushindwa kuangamia.

Aliwataka maofisa ugani na wataalamu mbalimbali wa kilimo, kuhakikisha wanawatembelea wakulima, na kuwapatia elimu juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu



Mratibu wa chanjo wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Jonathan Mollel (kulia), akitoa elimu kwa wasichana kutoshiriki tendo la ndoa wakiwa na umri mdogo na wazazi kushiriki kikamilifu kuhakikisha watoto wao wenye umri husika wanapata chanjo ya kinga ya saratani ya shingo ya kizazi, katika halmashauri hiyo, mkoani Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Dawa mimba utotoni Simanjiro yatajwa

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

WAKAZI wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kupambana na changamoto ya mimba za utotoni, kwa kuwasomesha watoto wa kike na siyo kuwaozesha wakiwa wadogo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Asia Ngalisoni, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusiana na changamoto hiyo.

Ngalisoni alisema wananchi wa wilaya hiyo wanatakiwa kupambana na tatizo hilo kwani baadhi ya watoto wa kike wanaachishwa masomo na wazazi na walezi wao, kutokana na kuozeshwa wakiwa wadogo kwa tamaa ya mali.

Alisema tatizo la mimba za utotoni linaweza kukomeshwa, kwa ushirikiano wa wazazi na walimu, kwani mtoto akikatishwa masomo watoe taarifa sehemu husika.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Silvanus Tairo, aliwataka wananchi hao kusomesha watoto wao, kwani kuna baadhi ya shule wanafunzi hawahitimu hata darasa la saba.

Tairo alitoa mfano wa Shule ya Msingi Lerumo, ambayo ilikuwa na wanafunzi 20 walioanza darasa la kwanza na mwaka jana waliandikisha kufanya mtihani wa darasa la saba walikuwa sita tu na ilipofika siku ya kufanya mtihani walipungua na kubaki watatu tu waliofanya mtihani huo.

Mkurugenzi wa Shule ya New Light, Mchungaji Sommy Severua, alisema, elimu ina nguvu mno kwani inaweza kusababisha mtoto wa kibarua akawa daktari bingwa.

"Mtoto wa kibarua anaweza kuwa bosi kutokana na ukubwa wa elimu aliyonayo, hivyo tunapaswa kuzingatia kuwapatia elimu watoto wetu badala ya kuwapeleka kwenye kuchunga mifugo au kuwaozesha wakiwa wadogo," alisema Mchungaji Severua.





## 80,000 wanufaika kampeni kupima TB na Ukimwi

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

WANANCHI 80,000 wa Wilaya ya Siha, wamenufaika na kampeni maalum ya upimaji wa Kifua Kikuu na Ukimwi, inayoendeshwa na jopo la madaktari wa Hospitali ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto (KIDH).

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusu kampeni hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo Dk. Riziki Kisonga, alisema kampeni hiyo inalenga zaidi kutangaza huduma za kinga dhidi ya kifua kikuu kwa umma.

"Hivi sasa kituo bado kinaendelea kupokea idadi ndogo ya walengwa ikilinganishwa na matarajio ya kupokea wagonjwa 300 wapya kila mwezi. Hili limesababishwa na wengine kushindwa kumudu gharama ya kufika kituoni," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kisonga, ili kutatua tatizo hilo, hospitali inaangalia namna ya kupata gari maalum la kuwafikia na kutolea huduma katika maeneo yao ya kazi.

Kwa sasa upatikanaji wa dawa muhimu katika hospitali hiyo ili kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na ambukizi, umeimarika kutoka asilimia 70 hadi asilimia 95 kwa mwaka 2019/2020.

Hospitalini ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto iko katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

"Tumeanza kuangalia ni jinsi gani tutaweka huduma thabiti na kuisambaza nchini kwa watu waliotibiwa ugonjwa wa kifua kikuu na kupona, lakini bado wanapata matatizo ya kuumwa kifua mara kwa mara ambayo ni sehemu ya magonjwa ambukizi," alisema Dk. Kisonga.

Alisema hospitali hiyo hivi sasa inaendelea kufuatilia mwenendo wa usugu wa vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu katika mikoa minne ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga.

**"Tumeanza kuangalia ni jinsi gani tutaweka huduma thabiti na kuisambaza nchini kwa watu waliotibiwa ugonjwa wa kifua kikuu na kupona, lakini bado wanapata matatizo ya kuumwa kifua mara kwa mara ambayo ni sehemu ya magonjwa ambukizi," alisema Dk. Kisonga.**

# Mkuu wa KKKT ahadharisha corona

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, ameagiza viongozi na waumini wa kanisa hilo nchini kote kutopuuza tahadhari za kitaalamu zinazotolewa ili kujikinga na kuthibiti kuenea kwa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Dk. Shoo alitoa maelekezo hayo katika Usharika wa Lyamungo Sinde uliopo Jimbo la Hai la Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, wakati akiongoza ibada ya maalum ya maombi ya toba dhidi ya virusi vya corona vinavyotikisa taifa na dunia kwa sasa.

"Tuchukue tahadhari zinazostahili dhidi ya ugonjwa wa corona, msifanye mzaha au utani... ugonjwa huu ni hatari na watu wanaangamia, tufuate maelekezo yanayotolewa na serikali na kumwomba Mungu katika jambo hili ili lipite," alisema.

Askofu huyo alitoa maelekezo hayo, wakati ugonjwa wa corona ukiwa umeanza kubadili taratibu za nyumba nyingi za ibada nchini ili kukabiliana na kusambaa kwa ugonjwa huo hatari.

Kwa sasa ibada za madhebu ya kikristo zimeanza kutawaliwa na elimu juu ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu Dk. Shoo aliwasihi Watanzania kote nchini kufuata maelekezo na tahadhari za kitaalamu zinazotolewa ili kujikinga na kuthibiti kuenea kwa virusi vya corona.

Aidha katika mahubiri yake, Askofu Shoo aliwataka wakristo wasiwe na hofu dhidi ya corona kuliko kumhofu Mungu.

"Fanyeni maombi kila saa na msisahau toba na kutambua kuwa Neema ya Mungu inatuwezesha kutambua kuwa Mungu ni mwenye huruma na anaona mahitaji yetu hata yaliyo madogo ya kiroho na kimwili," alisisitiza Dk. Shoo ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini.

Juzi, Rais John Magufuli akiwa jijini Dodoma, alisema kuwa hadi kufikia sasa watu 12 wamethibitika kuugua ugonjwa huo nchini, kati yake wanane ni Watanzania na wanne ni raia wa nje.




Mkuu wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Elizabeth Kitundu, akizungumza kuhusu mkakati wa kutokomeza ukatili wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watumishi waonywa utoro kazini kwa kisingizio corona

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

SERIKALI imewaonya watumishi wa umma wanaofikiria kuacha kwenda kazini kutekeleza majukumu yao kwa sababu ya tishio la ugonjwa wa corona, watakuwa wamekiuka sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Onyo hilo limo katika maelekezo yaliyotolewa kwa idara zote na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Renatus Msangira.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19) ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo, ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013.

Katika maelekezo hayo, ameagiza watumishi wa umma mkoani humo kutotumia janga hilo la kidunia kama njia ya kukiuka sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Msangira ambaye ni Katibu Tawala Msaidizi anayesimamia Utawala na Rasilimali Watu katika Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, alisisitiza ni kosa kwa mtumishi wa umma kutofika kazini au kutotimiza majukumu yake.

"Ni kosa kisheria kubaki nyumbani au kuendelea na shughuli zako binafsi kwa kusingizia tishio la ugonjwa wa corona au kujifanya unajikinga na corona kwa kukiuka sheria za utumishi wa umma. Ukifanya hivyo na ukabainika utakuwa matatani," alisema.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Kilimanjaro, Jonas Mcharo, akizungumza na watumishi wa umma katika kikao kilichoandaliwa kwa ajili ya watumishi wa mkoa huo kupata elimu muhimu ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona, aliwataka kutopuuza maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Credianus Mgimba, aliwataka watumishi wa umma kuacha woga, badala yake waendelee kutoa huduma kwa wananchi huku wakichukua tahadhari.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo. Dalili za ugonjwa huo huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 24, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI





Ukurasa 15

**Wataalamu wana-potafuta elimu ya kujitegemea kwa wastaafu**



Ukurasa 18

Kuwaacha kakakuona kutaitokomeza corona



Ukurasa 17

**2010-19 muongo uliozidi kiasi cha joto ulimwenguni**



# Watoto waacha masomo kisa, ngono, kandanda vibandani

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# Wananchi acheni kutumiwa kisiasa



IGP Sirro akizungumza na polisi wakati wa ziara yake. **PICHA ZOTE: JESHI LA POLISI.**

Ni ukweli kwamba taifa lolote duniani lenye maendeleo linachagizwa zaidi na msukumo wa uwepo wa amani na utulivu pamoja na utii wa sheria.

Amani ndiyo maendeleo, ni maisha hivyo chochote kinachofanywa kwenye jamii kinatokana na amani iliyopo kwenye eneo husika kwa mantiki kuwa watu wanapaswa kuitunza ili kufikia malengo wanayoyatarajia.

Mapema mwezi huu Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP Simon Sirro, anakutana na kuzungumza na baadhi ya wananchi wa eneo la Dareda mjini Babati mkoani Manyara, ambapo aliwataka kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo pia kuacha kutumiwa na baadhi ya viongozi wa kisiasa ili kuepuka kujiingiza kwenye vurugu zitakazopelekea uvunjifu wa amani.

Ziara ya IGP Sirro, anayoifanya mkoani Manyara ni miongoni mwa kazi zake za kawaida zenye kulenga kufanya ukaguzi, kuzungumza na maofisa na askari wa ngazi mbalimbali, kujua utendaji wao na utekelezaji wao wa majukumu ya kazi za kila siku za kipolisi na namna wanavyotoa huduma kwa wateja.

Hatua ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Sirro, kuzungumza na wananchi kila anapokuwa kwenye ziara zake za kikazi kinazidi kufungua ukurasa mwingine mpya zaidi hususan suala la ukaribu wa jeshi hilo na wananchi wake wa ngazi ya chini katika mrengo wa kuendelea kuhamasishana juu ya kuitunza amani ya nchi yetu.

Katika ziara hiyo, IGP Sirro anazungumza na wananchi na kuwataka wazazi na walezi kuendelea kuimarisha malezi ya familia zao kwa kuwajenga watoto kwenye maadili yanayofaa jambo ambalo litasaidia kuwaepusha kujiingiza kwenye matendo ya uhalifu na kuwa kero kwa wananchi.

"Niwatake wananchi wenzangu tuzingatie malezi ya watoto wetu kwani ni aibu kuwa na mtoto mwizi, na ni aibu pia kuwa na mtoto anayefanya vitendo vya ukatili," anasema IGP Sirro.

Anaiambia jamii kuwa inawajibu wa kutunza amani iliyopo sambamba na kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama huku akiwahamasisha watumiaji wa miundombinu ya barabara pamoja na vyombo vya moto kuendelea kutii na kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zinazoweza kuepukika.

Itakumbukwa kuwa, hivi karibuni IGP Sirro alifanya ziara ya ukaguzi katika jumla ya mikoa mitatu ikiwemo Manyara, Arusha na Kilimanjaro ambapo katika mikoa hiyo anazungumza na wananchi pamoja na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari na kutolea ufafanuzi masuala kadhaa kuhusiana na hali ya amani ya nchi yetu.

***Ofisi ya Uhusiano, Makao Makuu ya Polisi- Dodoma***

> Niwatake wananchi wenzangu tuzingatie malezi ya watoto wetu kwani ni aibu kuwa na mtoto mwizi, na ni aibu pia kuwa na mtoto anayefanya vitendo vya ukatili.



IGP Sirro akizungumza na wananchi katika mikutano mbalimbali wakati wa ziara yake.

SHAIRI

## Korona we ni nani? Unataka kitu gani?

Hasa watafuta nini? unatutesa kwa nini?
Utabaki hadi lini? watuachilia lini?
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

We' una mbaya harufu umekuwa maarufu,
Una sumu mara dufu, sote sisi twakuhofu,
Tumekuwa wadhaifu, watufanya tudhoofu,
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

Shule zote zimefungwa, miji yote imefungwa,
Vyuo vyote vimefungwa, maduka yameshafungwa,
Makanisa yamefungwa, misikiti imefungwa,
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

Unasafiri kwa kasi, zaidi ya mwendokasi,
Unasambaza mikosi, kila nchi haukosi,
Hebu tuambie basi, wataka ni' kwetu sisi?
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

Utadumu muda gani? utatokomea lini?
Hivi una nguvu gani? walikuumba na nini?
Tukusemee kwa nani? tukuseme kwa manani?
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?


Tumekukosea nini? kwako tumefanya nini?
Umeingia nchini, umeingia mjini,
Hadi kule kijijini, Korona sifa za nini?
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

Ukimwi hausikiki, Ebola haisikiki,
Malaria haisikiki, Taifodi haisikiki,
Kichomi hakisikiki, wengine hawasikiki,
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

Dunia imesimama, shughuli zimesimama,
Ofisi zimesimama, biashara zimesimama,
Kilimo kimesimama, uvuvi umesimama,
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

Leo mimi nashitaki, eti wajifanya konki,
Kwa Mungu ninashitaki, akupige na mkuki,
Mungu mtoe mkiki, tumia hata bunduki,
Korona wewe ni nani? unataka kitu gani?

**Issaya Lupogo**
**Mwalimu wa Kiswahili Chuo Kikuu Mzumbe,**
**(+255) 0712-143909**



Kirusi cha corona. **PICHA: MTANDAO.**

ELIMU

NA NIMI MWETA

# Wataalamu wanapotafuta elimu ya kujitegemea kwa wastaafu

WAHENGA walisema dunia ni mviringo, siyo tu kwa sababu ukizunguka dunia kwenda mashariki utaishia magharibi na mwishowe kurudi ulipotoka, ila kwa maana yake pana zaidi kimaisha.

Ndiyo hali inayoonekana katika suala zima la maana halisi ya Elimu ya Kujitegemea, kuwa kama ulivyo 'mtego wa panya,' wanaingia waliokuwamo na wasiokuwamo.

Awali walikuwa ni watoto wa shule wakifikia ujana waelekezwa kujitegemea si kutaka ajira mijini; sasa ni wastaafu.

Tena wastaafu wa kipindi hiki ndiyo zaidi walikuwa shule za msingi wakati wa Azimio la Arusha, ambako mada ya Elimu ya Kujitegemea ilifuata wiki kadhaa baadaye, ikiambatana na insha ya Ujamaa Vijijini. Machapisho hayo matatu kimsingi yaliweka kwa upana kiitikadi na kisera dhana nzima ya Ujamaa hapa nchini, hadi ilipoondolewa kimyakimya miaka ya 1990 mwanzoni. Ila insha hizo hazikuwahi kupoteza umaarufu wake licha ya kutekelezwa 'ndivyo sivyo' awali.

Kinachoshangaza ni jinsi mazingira ya kiuchumi na maisha kwa jumla hasa kuanzia miaka ya 1990 yalivyobadilika, na hatua kwa hatua kundi linalohitaji elimu ya kujitegemea linakuwa si la vijana tena, ila wazee.

Suala ni kwamba kwa upande wa vijana suala la kujitegemea lilikuwa mwelekeo wa ziada kwa kile ambacho walikuwa wanakitafuta, yaani kuendelea na masomo hadi sekondari na hata elimu ya juu. Endapo wasingefika hapo, wasione ni mwisho wa matumaini.

Hivyo elimu ya kujitegemea haikuwa inahoji mwelekeo wa kuinuka kimaisha kupitia elimu ila dhana kuwa bila ajira ya ofisi suala zima la kwenda shule ni kama lilikuwa halina maana.

Hali hiyo ilikuwa tayari inaleta mvutano kijamii kwani mwaka 1968, ambako mazingira yanafanana na kipindi insha ya Elimu ya Kujitegemea inaandikwa, ni watoto 13 tu waliokuwa wanaingia sekondari pindi wakimaliza shule ya msingi. Familia zilikuwa zinawaona wamefeli kimaisha, n.k.

Kwa maana hiyo elimu ya kujitegemea aina ya kwanza, au maana yake halisi, ni kutumia elimu ya msingi (hadi kumaliza madarasa ngazi hiyo) kama njia ya kuelewa stadi za maisha, ikiwamo kilimo, ufundi wa ngazi tofauti na hasa unaohusu ujenzi, uashi, cherehani, randa, plau, kilimo bora, n.k. Jitihada hizo zilitakiwa ziwe sehemu ya mafunzo shuleni ili wanafunzi wakimaliza ngazi hiyo ya maisha waendelee na uelewa huo vijijini. Wasianze kukata tamaa kwa 'kufeli.'




Mzee mstaafu akisaidiwa kupata huduma mbalimbali. **PICHA: MTANDAO**

> Si umaskini kwa jumla ila kustaafu, na kuondoa hali hiyo kinachohitajiwa siyo tena stadi za maisha kwani zinahitaji uwezo wa kufanya kazi.

Stadi hizo kimsingi zimeendelea kuwa muhimu ila hazianzii moja kwa moja shule za msingi ila baada ya hapo, licha ya kuwa baadhi ya masomo ya stadi za maisha yaliingizwa hatua kwa hatua katika mitaala. Baadhi ya wataalamu wanaona hatua hiyo ilisaidia kuvuruga uelewa na undani wa kufikiri wa wanafunzi, kwani muda ambao ungetumiwa kuitafakari dunia, sayansi au historia unatumiwa kujifunza na kushona. Si mwanafunzi atajifunza kivyake baada ya shule, akitafuta maisha?

Katika miaka ya 1990 wakati serikali inapunguza idadi ya wafanyakazi enzi za kuanza kutumika kwa kompyuta na kuondolewa 'mafaili' lukuki katika maofisi, umuhimu wa stadi za maisha ndipo ulipoanza. Ila haukujikita katika akili au hisia za watu wa njia hiyo, ila kama shughuli za kibiashara, na ghafla Tanzania ikaanza kuwa taifa la wachuuzi wadogo wadogo wanaokaa mijini. Sehemu ya bidhaa, hasa mazao na mbogamboga ilikuwa inatoka vijijini, na nyingi zaidi kutoka viwandani mijini na nyingine kutoka nje, hasa mitumba - eneo pana zaidi la ajira ya vijana.

Walioendelea kufanya kazi katika sekta ya umma na hata binafsi hatua kwa hatua wakaingia katika biashara, hasa baada ya kuondolewa 'miiko ya uongozi' kupitia Azimio (au |Tamko) la Zanzibar, 1991. Ilikuwa ni hatua ya pili ya kuondoa mfumo wa Ujamaa kwanza ikiwa ni kulegeza masharti ya kuingiza bidhaa nchini au kuuza nje, ikiendana na kuondolewa kwa vijiji vya ujamaa, kila mtu alime kivyake. Hatua ya pili ikawa ni ubinafsishaji, kulegeza upatikanaji wa fedha za kigeni, na kuruhusu waajiriwa kumiliki biashara.

Kinachoonekana katika mada za miaka ya karibuni kwa mfano mijadala kuhusu mifumo ya kuondoa akiba baada ya kuacha kazi, ni hali halisi kuwa wanaofikia umri wa kustaafu mara nyingi zaidi wanauona umaskini ukiwanyemelea. Ina maana hapakuwa na uwezo wa kutosha miongoni mwa wafanyakazi walio wengi kuingiza fedha katika shughuli za ziada ambazo zinawakinga na umaskini,na hiyo ni kweli kwa walio wengi. Licha ya kuwa watalaamu wanasema kuwa wengi waliwekeza katika familia zao, kudai umaskini unatoka hapo ni kuongeza chumvi.

Kutokana na hulka ya kawaida ya kuoneana haya, mhadhiri Dk. Godson Lema wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi hakuzungumzia kuna uhusiano gani kati ya starehe za ujana na hata utu uzima, na umaskini uzeeni.

Umaskini umekuwa ukizungumziwa zaidi kuhusu wanawake na watoto, na kwa kiasi fulani vijana ingawa hapo kinachojadiliwa ni ajira na siyo umaskini wenyewe - wakati hali ya wazee inakuwa somo tofauti.

Si umaskini kwa jumla ila kustaafu, na kuondoa hali hiyo kinachohitajiwa siyo tena stadi za maisha kwani zinahitaji uwezo wa kufanya kazi. Ni mpangilio sahihi wa kustaafu, kujiwekea akiba, n.k.

Hapo, kuna kitendawili kwani mishahara wanayopata walioko kazini, hata wa ngazi za juu, haitoshi kuweka akiba inayoweza kutumika kwa njia endelevu? Suala hapa ni kujiwekea mazingira ya kuwa na uwezo wa kumudu maisha ya kijijini baada ya kustaafu, kwa kuwa na nyumba, shamba na mifugo, na itazamiwe kuwa maji pia yatakuwa yanapatikana.

Ila mtu anaweza kujizalishia chakula, huku bei ya mazao kama mbogamboga pale ambapo kuna soko, ni ya kutupa, isiyofaa mstaafu jijini.

ELIMU

**NA ELIZABETH ZAYA**

VIBANDAUMIZA MITAANI

# Watoto waacha masomo kisa, ngono, kandanda vibandani

KATIKA kata ya Kimanzichana mkoani Pwani, kilio cha wananchi kwa sasa pamoja kuogopa kusambaa kwa virusi vya korona, wanatatizwa na kuanzishwa kwa utitiri wa vibanda vya video mitaani, vinavyoonyesha burudani lakini pia picha za ngono kwa watoto wadogo na wanafunzi.

Sehemu hizo za burudani maarufu kama vibanda umiza pamoja na kuonyesha kandanda na tamthilia, vinaelezwa kuwa vimegeuka hatarishi kwa maisha ya watoto baada ya baadhi kukimbia shule na kushinda vibandani wanapojifunza mambo mengi yakiwamo masuala ya ngono.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakati ilipotembelea Kimanzichana, wakazi hao wanasema pamoja na lengo zuri la ujio wa vibanda hivyo ni janga kwa watoto ambao hawazingatii shule.

Sihota Mchonjo, mjumbe wa serikali ya mtaa wa Lisimalike anaeleza kwamba katika siku za hivi karibuni kumeibuka kundi la watoto ambao wengine ni wanafunzi wanaoshinda katika vibanda vya video na hivyo kushindwa kusoma.

Mchonjo pia anasema mbali na kuonyesha burudani ikiwamo mpira, lakini vibanda hivyo vimekuwa vikionyesha picha za ngono ambazo hazifai kwani hupoteza watoto wadogo.

"Kwa kweli tunaomba serikali itusaidie , watoto wetu ni wadogo kushinda katika vibanda 'umiza' yaani kuanzia saa 4:00 asubuhi unakuta wamefungua na watoto wamejaa tele wengine ni wanafunzi tena tunawafahamu, hii si sawa kimalezi na kwa maendeleo ya taifa."anasema Mchonjo.

"Wanatudanganya kwamba wanaonyesha mpira na tamthilia tu, lakini ni waongo, wanaweka hata picha za ngono na watoto nao wanaangalia. Kwa mfano kama mpira ni saa 10 jioni, wanachofanya kabla ya muda huo, wanaanza kuonyesha vitu vingine. Kwa hiyo mpaka mtoto atoke humo anakuwa ameangalia vitu vingi vya ajabu na tunawaona watoto wanabadilika kidogo kidogo kila siku," anasema mjumbe huyo.

Diwani wa Kata ya Kimanzichana, Ally Kassim Ndipitipi, anasema baada ya kubaini tatizo hilo la watoto kushinda katika vibanda hivyo na wengine wakiwa wanafunzi alitoa taarifa katika Ofisi ya Mtendaji.

"Tatizo hili lipo hapa tunahitaji kulikomesha kwa sababu bila kufanya hivyo tunaharibu watoto wetu na tunazalisha kizazi cha ajabu,"anaonya Ndipitipi



Jamii kufuatilia matukio kwenye video kwa ajili ya kujifunza ni mambo ya kawaida katika baadhi ya maeneo ili kufikisha ujumbe kwa umma unaohusisha watoto na watu wazima. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> "Wanatudanganya kwamba wanaonyesha mpira na tamthilia tu, lakini ni waongo, wanaweka hata picha za ngono na watoto nao wanaangalia.



Wanafunzi kusoma kwenye madarasa yasiyo na kiwango ni moja ya changamoto zinazowafanya kutoroka shuleni na kukimbilia kwenye mabanda ya video mitaani.

### UTORO SHULENI

Nipashe lilifika katika shule moja ya msingi katika kata ya Kimanzichana na kuzungumza na mkuu wa shule hiyo, Adrian Tete, anayekiri baadhi ya wanafunzi hutoroka na kwenda katika vibanda hivyo na kwamba tayari walisharipoti suala hilo katika ofisi ya kijiji na ya mtendaji kata.

"Baadhi ya wanafunzi wakati mwingine kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, hulazimika kusubiriana nyakati za kuingia darasani, kwa hiyo katika kipindi hicho unakuta wametoroka na kwenda kwenye vibanda hivyo vya video,"anasema Tete na kuongeza:

"Tatizo hili lilianza kuwa kubwa na ikabidi tutoe taarifa kwenye mamlaka zinazohusika ikwamo ofisi za kijiji na za mtendaji, mpaka sasa hali imepungua japokuwa bado kuna wachache wanaoendelea kutoroka ambao tunapambana nao na baadhi yao tumewaita walezi na wazazi wao."

Anaeleza kuwa wenye video wanafanya shughuli hizo kihalali, lakini inabidi mamlaka zinazohusika ziliangalie suala hili la kuruhusu watoto kuingia humo hasa nyakati ambazo wanatakiwa kuwa darasani kusoma.

### WATOTO WANABETI

Mwenyekiti wa kamati ya shule iliyotembelewa ,Mohamed Mazoea, anasema taarifa hiyo ilifika hadi katika vikao vya kamati ya shule na tayari walilizungumzia suala hilo na kuripoti katika mamlaka zinazohusika.

"Huku kwetu tunalia sana na wazazi na walezi, kweli wanashindwa kuwalea watoto wao vizuri, kuna kipindi tulipata hadi kesi ya wanafunzi kutoroka kwenda kwenye hivi vibanda vinavyotumia katika michezo ya kubeti au kubashiri, ilituchanganya kweli na ilibidi tutumie nguvu kubwa sana kumpambana nao mpaka tumefanikiwa na sasa wameondoka,"anasema Mazoea.

### UKAGUZI KUSHTUKIZA

Mtendaji wa Kata ya Kimanzichana, Said Abdalah Said, anasema baada ya suala hilo kufikishwa katika ofisi yake waliitisha kikao cha kamati ya shule pamoja na kushirikisha baadhi ya viongozi wa kata hiyo pamoja na kulifikisha katika kituo cha polisi cha Kimanzichana.

"Na Jeshi la Polisi lilichukua hatua kadhaa ikiwamo kuanza kufanya ukaguzi wa kushtukiza ambush 'ambush' katika vibanda mbalimbali,"anasema Said.

Anaeleza kuwa hawawezi kuwazuia wenye vibanda wasifanye biashara kwa sababu nao wanafanya uwekezaji huo kisheria, lakini wanachotaka wazingatie sheria, siyo kwenda kinyume na vibali vyao.

### MAONI YA WANAFUNZI

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wanakiri kuwapo kwa baadhi yao kutoroka na kwenda kwenye vibanda hivyo.

"Ni kweli kuna baadhi ya wanafunzi wanatoroka kwenda kwenye hivyo vibanda vya video na hulipia Sh.100 kwa muda wote wanaokaa humo,"anasema mwanafunzi mmoja wa darasa la saba katika shule hiyo ambayo jina linahifadhiwa.

Anaongeza: "Nina wadogo zangu ambao wanasoma hapahapa ambao hutoroka na wanakwenda huko, na mama yangu ameongea mpaka amechoka, kila siku anawakataza lakini hawasikii na wakirudi wanasimulia kila kitu wanachokiona huko na vingine wanavyoviangalia kwenye vibanda ni vya aibu."

Mwanfunzi huyo anasema kuna siku aliwafuata watoto hao baada ya giza kuingia na alipoingia alikuta wanaonyesha picha za ngono, akawabeba na akawasemea kwa wazazi wao.

### SHULE NYINGINE

Mkuu wa Shule, Victor Marisha, mwalimu katika shule jirani, anasema tatizo la watoto kutoroka na kwenda katika vibanda vya video ni miongoni mwa matatizo yanayowatesa.

"Hili linatutesa sana katika shule yetu, tumelazimika kuunda timu ya wanafunzi wenye nidhamu ambao wamekuwa wakishirikiana na mwalimu wa nidhamu kwenda kuwafuatilia wanafunzi wanaotoroka kwenye vibanda hivyo, na tumesharipoti kwenye uongozi wakijiji,"anasema Marisha.

### USTAWI WA JAMII

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mkuranga, Foibe Peter, anasema watoto kushinda kwenye vibanda vya video katika halmashauri hiyo ni kubwa na wamekuwa wakipambana nalo mara nyingi.

"Hilo tatizo haliko sehemu moja tu, karibu kila sehemu ya Mkuranga kuna shida hiyo na linatutesa sana huku, na limechangia kwa kiwango kikubwa kuharibu watoto kwa sababu huko ndiko wanajifunza mambo ya ajabu kweli kweli,"anasema Peter.

Anaongeza kuwa watoto wanajifunza mambo mabaya na kupotoka kwenye vibanda umiza na tatizo kubwa hata wanapotoa elimu kwa jitihada zote wazazi nao hawatekelezi wajibu wao hivyo kuwapa walimu mzigo mkubwa .

Anasema tatizo jingine linalochangia watoto katika eneo hilo kujifunza mambo mabaya ni pamoja na wazazi kutengana na kukosa malezi ya pamoja, watoto kuishi na bibi zao ambao wengi wao hawana nguvu ya kuwafuatilia.

> Na Jeshi la Polisi lilichukua hatua kadhaa ikiwamo kuanza kufanya ukaguzi wa kushtukiza ambush 'ambush' katika vibanda mbalimbali

### WENYE VIBANDA

Mmiliki wa kibanda cha video au kibanda umiza katika eneo la Kimanzichana ambaye alikataa kutaja jina lake, anasema hawawalazimishi watoto kuingia katika vibanda hivyo, isipokuwa wenyewe ndiyo hulazimisha kuruhusiwa kuingia na kutizama picha.

"Sisi tunafahamu masharti tuliyopewa ya kufanya biashara hii, hatuwezi kulazimisha watoto waingie isipokuwa watoto wenyewe ndiyo wabishi. Unakutana na katoto kanakuja kanalazimisha, ukikakataza kanakwambia mbona mama ameniruhusu na amenipa hela ya kuingilia wewe ni nani unanikataza? Wengine wanakuja na mzazi kwa hiyo ongeeni na wazazi wao wawakataze na siyo kutulaumu sisi,"anasema.

### OFISI YA UTAMADUNI

Ofisa Utamaduni Halmashauri ya Mkuranga, Boppe Kyungu, anasema sheria ya utamaduni inawataka wamiliki wa vibanda vya video kuonyeshwa kuanzia saa 10 jioni.

"Hakuna sheria inayoruhusu vibanda vya video kufunguliwa kabla ya saa 10 jioni, lakini pia sheria ndogo ya halmashauri hairuhusu watoto chini ya umri wa miaka 18 kuingia kwenye vibanda hivyo, wanakiuka utaratibu kwa sababu hata vibali walivyopewa havionyeshi hivyo," anasema Kyungu.

RIPOTI

# 2010-19 muongo uliozidi kiasi cha joto ulimwenguni



Hali ya madhara ya mabadiliko ya tabianchi katika anga, ardhi na baharini. **PICHA: UN**

DALILI za mabadiliko ya tabianchi kama vile ongezeko la joto la ardhini na baharini, kuongezeka kwa kina cha bahari na kuyeyuka kwa barafu, ni mambo yaliyoangaziwa kwa kina katika ripoti mpya ya Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa Duniani ((WMO) na wadau wengine, iliyotolewa mwezi huu jijini New York Marekani na Geneva Uswisi.

Ripoti inaeleza kuwa kuna ongezeko la ishara na madhara ya mabadiliko ya tabianchi katika anga, ardhi na baharini.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa kuna madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, afya ya binadamu, uhamiaji na ukosefu wa makazi, uhakika wa chakula, ardhi na maisha ya viumbe vya majini.

Aidha, ripoti hii inathibitisha taarifa iliyotolewa awali wakati wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN), wa mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Desemba mwaka jana kuwa, mwaka huo wa 2019 ulikuwa wa pili kwa kuwa na joto la juu katika rekodi ambapo mwaka 2015 hadi 2019 ni miaka mitano iliyokuwa na joto zaidi katika rekodi za joto huku mwaka 2010 hadi 2019 ni muongo uliorekodiwa kuwa na joto la juu zaidi ulimwenguni.

Tangu mwaka 1980, kila muongo umekuwa na joto la juu zaidi ya muongo uliotangulia tofauti na ilivyokuwa kwa miongo mingine ya kuanzia mwaka 1850.

Mwaka 2019 ulikamilika na wastani wa joto la dunia la nyuzi joto 1.1°C juu ya makadirio ya viwango vya kabla ya mapinduzi ya viwanda, rekodi ya pili baada ya ile ya mwaka 2016 wakati ambapo tukio la El Nino lilichangia katika ongezeko la joto juu ya mwenendo wa Jumla wa ongezeko la joto.

Taarifa hiyo ya WMO kuhusu hali ya tabianchi ya ulimwenguni kwa mwaka 2019 inajumuisha mchango wa taaarifa kutoka mamlaka za hali ya hewa na maji za mataifa mbalimbali, wataalamu wa kimataifa, taasisi za sayansi na mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Ripoti hiyo inatoa taarifa muhimu kwa watunga sera kuhusu umuhimu wa kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, akizungumzia taarifa hiyo kupitia dibaji ya ripoti hiyo ananukuliwa akisema, "kwa sasa tuko nyuma ya muda katika mbio za ama kufikia lengo la nyuzi joto 1.5 au 2 ambazo Mkataba wa Paris unatolea wito."

Halikadhalika, Katibu Mkuu wa WMO Petteri Taalas anasema, "kwa kuwa viwango vya hewa chafuzi vinaongezeka, ongezeko la joto litaaendelea. Utabiri wa hivi karibuni unaonesha kuwa rekodi mpya ya mwaka ya dunia inaweza kutokea katika miaka mitano ijayo. Ni suala la muda." **HABARI ZA UN**

JE, WAJUA?

# Kuwaacha kakakuona kutaitokomeza corona



KUIBUKA kwa kirusi cha corona huko China kunaaminiwa na wataalamu kuwa kutaokoa maisha ya kakakuona ambao walikuwa hatarini kutoweka.

Nyama ya kakakuona inahusishwa kuwa chanzo cha kirusi hicho kinachosababisha mafua makali yanayoua kwa muda mrefu, licha ya kwamba utafiti unaendelea. Kirusi hicho kipya kilichopewa jina COVID19 baada ya kudhibitiwa nchini China ni wazi usalama wa kakakuona unarejea kwa sababu mnyama huyo alikuwa analiwa na kuchukuliwa kama maalum na mahsusi katika nchi za China na Asia.

Kwa mujibu wa mtandao wa Televisheni ya AlJazeera hadi Jumamosi iliyopita watu 12,000 walikuwa wamepoteza maisha, wengine 299,000 wameugua , na kati yao 91,500 wamepona kwa mujibu wa takwimu za Chuo Kikuu cha Johns Hopkins cha Marekani, kilichonukuliwa na mtandao huo.

China mwezi huu ilitangaza marufuku ya kula nyama ya kakakuona au 'pangoline' kutokana na kuhusishwa na kirusi hicho.

Kakakuona mnyama mwenye magamba mengi na yenye muonekano wa kipekee anatajwa na taasisi ya kimataifa ya the International Union for Conservation of Nature (ICUN), kama aliyehatarini kutoweka kwani hupendwa na kuchukuliwa kama chakula cha kipekee na cha gharama kubwa kwa China na mataifa yote ya Kusini Mashariki mwa Asia zikiwamo Indonesia na Malyasia.

Hatua hiyo inakuja baada ya utafiti kuuhusisha ugonjwa wa homa ya corona na nyama ya kakakuona maradhi yakianzia kwenye soko la nyama la Wuhan nchini China, hivyo serikali ikapiga marufuku ulaji wa wanyama wa porini wakiwamo kakakuona.

Licha ya kwamba kwa Tanzania kakakuona ni mnyama wa amani, baraka na furaha kwa mataifa ya Asia hasa China ni kitoweo cha thamani kubwa , huku magamba yake yakitumiwa kutengeneza dawa za asili.

Marufuku hiyo inalenga kukomesha usambaaji wa virusi ambavyo vimeambukiza watu zaidi ya 290,000 dunia nzima na wengine zaidi ya 12,000 kufariki dunia . Hivyo wanyama hao watanusurika na wengine wengi watapona kama katazo hilo litadumu kwa muda mrefu.

"Ninashangilia katazo hili kama tunavyoona serikali ya China imeamua na kujizatiti kubadilisha desturi hii ya miaka mingi ambayo haina mashiriko kwenye jamii ya sasa zinazoishi maisha ya kisasa," anasema Jeff He, Mkurugenzi wa the International Fund for Animal Welfare na kuongeza kuwa ni hatua mujarabu katika kulinda wanyama pori wa China na duniani.

### WATAWEZA?

Katika mlipuko wa kirusi cha mafua ya ndege (SARS) china ilipiga marufuku ulaji wa ndege pori kama inavyofanya sasa kwa kakakuona na wanyama wengine, lakini SARS iliyotikisa kwenye 2003 baada ya kudhibitiwa Wachina wanaendelea kula ndege pori kama popo na nyoka.

"Nadhani serikali imeona kwamba kodi na makusanyo mengine yanayotokana na biashara ya wanyama na ndege hao hauna tija ukilinganishwa na ustawi wa jamii na uchumi wa China, "anasema He.

### KWA NINI KAKAKUONA

Mnyama huyo ambaye anauzwa na kusafirishwa kwa njia haramu sehemu nyingi duniani nyama yake inasifika kwa ladha na magamba yake kuhusishwa na dawa yakitajwa kuwa yana tiba.

Peter Knights, Mtendaji Mkuu wa taasisi ya kulinda wanyama pori ya WildAid charity, inasema inalikaribisha katazo hilo ambalo pia ni mafanikio katika juhudi za kimataifa za kulinda na kuhifadhi wanyama hasa kakakuona.

"Swali tunalobaki nalo ni hili mambo yataendelea hivi kwa muda gani?? Tunaamini kuwa China itaisaidia kuendesha kampeni za kufunga masoko ya wanyama pori dunia nzima," anasema.

Mlipuko wa corona uwe onyo uamshe binadamu kutunza na kuhifadhi vitu na viumbe asilia vinginevyo waangamie au kupata madhara makubwa kiafya na kiuchumi kama ilivyotokea athari za corona.

"Kama tukisikia na kusimamia maonyo tutalinda na maisha ya binadamu na wanyama kama kakakuona," anasema Kinights.

Biashara ya kakakuona ilipigwa marufuku mwaka 2016 na mkataba wa kimataifa wa kulinda wanyama walio katika hatari ya kutoweka CITES, Katibu wa CITES Ivonne Higuero, analikaribisha katazo la China la biashara ya wanyama hao.

Biashara haramu ya wanyamapori inakadiriwa kufikia wastani wa Dola bilioni 15 kila mwaka kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Kimataifa la Kulinda na Kuhifadhi Maumbileasilia WWF, ikiyataja zaidi masoko ya Asia ambayo yanaihusisha China.

## NYUMBA YETU

# Ni vyema kuifahamu sementi unayojengea

ZAMA hizi kila mmoja anatamani kuwa na nyumba yake akiamini kuwa maisha ya mjini ukiwa na mahali pako binafsi pakulala ni bora zaidi kuliko kupanga.

Kwa hiyo ni vyema kufahamu kuhusu sifa na viwango vya sementi ambayo ndiyo inayotumiwa kwa nchi kujenga ambazo kila mmoja anatamani kuwa nayo, ili unapojenga uwe na makazi bora ambayo ni nyumba imara.

Mtandao wa 'Ujenzi Connect' unafahamisha masuala mbalimbali kuhusu ujenzi na moja ya swali unalouliza ni hili, " Unafahamu nini ukinunua Simenti imeandikwa 32.5N au 42.5N?

Jibu ni kwamba unachoona hapo ni masuala ya ubora tofauti wa simenti unayouziwa , ukieleza kuwa sementi zina madaraja matatu.

Mtandao unadokeza kuwa kuna madaraja matatu ya ubora au uimara wa simenti ambayo ni uimara wa chini 32.5, mwingine ni bora zaidi ya ule wa chini 42.5 na uimara wa juu zaidi unaopewa alama 52.5. Semeti ya gredi 52.5 bado haijaanza kuzalishwa kwa soko la Tanzania, ikimaanisha kuwa kuna gredi ya 32.5 na 42.5 tu.

Sementi ya daraja la chini la ubora ni asilimia 32.5 na inafaa zaidi kwa matumizi ya kupiga plasta na kazi ndogo ndogo na ile ya daraja la juu zaidi yenye alama 42.5 inafaa zaidi kwa kazi za zege kama kutengeneza nguzo, bimu, slabu na kujenga madaraja kutokana na uimara wake kuwa mkubwa zaidi.

Kwa baadhi ya nchi wana simenti ya uimara wa juu zaidi ya kipimo cha 52.5. Kwa ujumla sementi hutumika kwa kutengenezea matofali, kutengeneza plaster na kupiga plasta, kusakafia, kuziba nyufa, kuunganisha matofali kutengeneza ukuta na kutengeneza zege.

Ukifika dukani kununua sementi ikiwa na mifuko yenye maandishi ya ubora alama 32.5N, 32.5R, 42.5N, 42.5R au hata 52.5N. Hizi herufi 'N' au 'R' hazina maana yeyote zaidi ya kuelezea kipindi cha mapema zaidi (umri) kwa simenti kuanza kufikia ubora wake ukipimwa katika siku mbili hadi wiki moja.

Ni bahati nzuri Tanzania sasa ina viwanda vingi vya kuzalisha sementi ambavyo hutambulika kwa majina mbalimbali na kwa wingi huu wa wazalishaji huleta nafuu kwa walaji kupitia ushindani wa soko kibiashara.

Hivyo ni vizuri kutafuta sementi yenye alama za juu kulingana na kile unachokwenda kufanya kwa sababu uimara wa tofali, zenge, nguzo, madaraja ya barabara, makalavati na plasta unategemea sementi uliyotumia iwapo ni 42.5N au 32.5.

Mtandao unatoa angalizo kuwa tabia moja ya zege ambao ni mchanganyiko wa kokoto, mchanga na simenti katika uwiano uliopimwa na kuchanganywa na maji huendelea kuwa bora kadiri siku zinavyoongezeka.

Katika upimaji na uchanganyaji wa zege, ubora hupimwa baada ya siku saba kuona kama kuna uwezekano wa kufikia ubora unaotarajiwa huko baadae.

Kipimo cha siku saba kikionyesha kuwa na majibu ya mwelekeo mbaya zege husika inabomolewa. Hufuatia kipimo baada ya umri wa siku 14 na baadae siku 28 kuhitimisha kwamba viwango vya ubora vitafikiwa kadiri umri wa zege unavyoongezeka.



Sementi tayari kwa kuzalisha matofali na kazi nyingine za ujenzi. **PICHA: MTANDAO.**

UCHAMBUZI

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Kutojali mazingira asilia kunavyoweka dunia hatarini


DUNIA tangu kuumbwa ilikuwa eneo bora lenye vitu mbalimbali kuanzia nchikavu, sehemu zenye maji kama maziwa, mabwawa, mito, bahari na ardhioevu (wetlands).

Juu ya nchikavu kuna jamii nyingi za misitu yenye aina mbalimbali za miti na mimea pamoja na wanyamapori na bioanuai nyingine nyingi.

Baharini wapo samaki na viumbe wengine wengi, kadhalika angani kuna ndege aina mbalimbali na hewa yenye mchanganyiko wa gesi mfano, nitrogen, oxygen na carbon dioxide (gesiukaa).

Yote hayo, kwa ujumla wake, ndiyo mazingira asilia kwa manufaa ya binadamu. Hivyo kutunza na kulinda mazingira ni kushukuru na kuheshimu kazi nzuri aliyoifanya Mungu.

Vitu vyote alivyoviumba na kuvitengeneza alimkabidhi binadamu kuvitumia, mali na rasilimali mbalimbali vikiwamo viumbe hai vya majini, ndege warukao angani, misitu na mimea, wanyamapori na wadudu kama senene na kumbikumbi.



Ulinzi wa mazingira ya asilia kama misitu ni kipaumbele kwa dunia salama . **PICHA: MTANDAO.**

**ULINZI WA UUMBAJI**

Baadhi ya viongozi wakuu duniani wanaoguswa na suala la mazingira ni Papa ambaye mwaka 2017 Papa Fransisko wa 16 alitoa Waraka wa Kichungaji unaojulikana kama: "Laudato Si", na kutahadharisha kuhusu umuhimu wa mazingira kwa maisha.

Anasema: "Mazingira yetu ni kama dada tunayeshirikiana maisha na mama mzuri anayeinyoosha mikono yake ili kutukumbatia". Hata hivyo, hali ya sasa ya mazingira duniani siyo nzuri kama ilivyokuwa miaka 50 iliyopita.

Ingawa tunasingizia ongezeko kubwa la watu lakini pia matumizi yetu kwa mazingira hayaendani na tahadhari kuhakikisha kuwa hatuyaharibu bali tunatumia kwa uangalifu mkubwa kwa kuishi kirafiki na mazingira.

Kwa uelewa kwamba bila kuwepo mazingira imara hali ya maisha inayuba. Ni kweli wanadamu tumeongezeka sana kufikia zaidi ya billion saba lakini ongezeko hili lisiwe sababu ya kuendelea muharibu mazingira asilia kwa mtazamo wa "kuganga njaa"; maana kwa kufanya hivyo tunajenga ufa mkubwa kwenye mfumo mzima wa kiikolojia hadi kuhatarisha uhai wetu na wa viumbe wengine.

Waraka wa Papa Fransisko, siyo tu kutukumbusha wajibu wetu kwa mazingira bali pia unatusisitizia kuwa ardhi ni mama anayetudumisha na kutufanya tuishi na anayezaa matunda yake mbalimbali na yenye rangi za kupendeza pamoja na mimea kadhawakadha ikistawi sehemu mbalimbali nchini kwa matumizi na faida ya binadamu na wanyamapori pamoja na mifugo yetu

> Kulingana na hali halisi ilivyo nchini mazingira asilia sasa yanaanza kutugeuka na kutuadhibu kwa sababu ya uharibifu ambao tumekuwa tukiufanya kwa miaka mingi iliyopita.

Mazingira yaliyotunzwa vizuri ni kama chemichemi inayobubujika maji muda wote. Hii inamaanisha kwamba iwapo hali ya mazingira asili haitavurugwa na shughuli za kibinadamu tutapata maji ya kutosha na mvua zitanyesha kwa wakati muafaka (kwa majira yake).

Kulingana na hali halisi ilivyo nchini mazingira asilia sasa yanaanza kutugeuka na kutuadhibu kwa sababu ya uharibifu ambao tumekuwa tukiufanya kwa miaka mingi iliyopita.

Nchi zilizoendelea nazo siyo salama maana kumekuwepo na matukio ya maafa ya mara kwa mara. Hali hiyo ni ishara kuwa hali ya mazingira imekuwa siyo shwari tangu enzi za mapinduzi ya viwanda (industrial revolution) kwenye nchi zilizoendelea.

Wakati nchi yetu inaathirika na matukio kama ya ukame na mafuriko hadi kupata mvua nyingi nje ya mfumo (mfano kunyesha na kusababisha mafuriko ya aina yake miezi ya Januari na Februari 2020 siyo hali ya kawaida.

Wakati huohuo nchi zilizoendelea zimekuwa zikikumbwa na matukio ya vimbunga pamoja na mioto kichaa kuteketeza maeneo makubwa ya misitu na mali za watu. Mfano, moto uliozuka mwezi Januari 2020 nchini Australia na kusababisha hasara kubwa sana kwa jamii na serikali.

**GESI ZENYE ATHARI**

Ongezeko kubwa la shughuli za viwanda kwa nia ya kujenga uchumi imara limepelekea balaa la kiikolojia kutokana na usalishaji wa gesiukaa ($CO_2$) nyingi inayochangia, kwa kiasi kikubwa, ongezeko la joto duniani.

Tangu 1992 viongozi wakuu wa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa wanaounda mpango wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi,

"United Nations Framework Convention on Climate Change" (UNFCCC) pamoja na wataalam waliojikita kwenye masuala ya mabadiliko ya tabianchi wamekuwa wakikutana kutafuta muafaka juu ya ongezeko la joto duniani.

Ni takribani miaka 27 imepita lakini bado hatujapata suluhu juu ya changamoto hiyo. Kwa mtazamo wangu hali inakuwa hivyo kutokana na ubinafsi na kujali zaidi ongezeko la uchumi pamoja na mataifa yaliyoendelea kuwa na mtazamo kwamba ni changamoto ambayo wanaweza kuimudu vizuri zaidi lakini bila kujali athari zake kwa mataifa mengine.

Hata hivyo, Papa Fransisko kupitia andiko la mazingira anatutahadharisha kuwa "hakuna kitu chochote duniani kisichotuhusu, kwa mtazamo huo suala la ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi ni changamoto zinazohusisha mataifa yote hata kama limeendelea sana maana katika harakati za kuendelea zinachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la joto na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa kuwa dunia sasa inakabiliwa na tatizo la uharibifu mkubwa wa mazingira, hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu na mataifa yote kwa ujumla; kuchukua tahadhari bila kujali viwango vya maendeleo na nguvu za kiuchumi walizonazo.

**KUTIMIZA WAJIBU**

Mamlaka zilizopo zijitahidi kudhibiti shughuli za kibinadamu zinazosababisha kuhatarisha uhai wa mazingira.

Mfano, wakulima nchini kulima hadi kufikia kingo za mito au kuanzisha makazi kwenye maeneo hatarishi ikiwamo mabondeni na njia za wanyamapori (shoroba).

Elimu ya mazingira na namna ya kuishi kirafiki na mazingira itolewe na iwe endelevu. Mkazo uwekwe kwa vijana wote walioko shuleni, kwenye vyuo na walioko mijini na vijijini. Jamii yote isiachwe nyuma maana elimu ya mazingira ni muhimu kwao ili mkulima atumie mbinu endelevu kufanikisha lengo lake, kupata chakula cha kutosha au mazao ya biashara bila kuathiri misingi asilia ya ikolojia.

***Dk. Felician Kilahama ni Mwenyekiti, Wildlife Conservation Society of Tanzania (WCST)***



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Mimba shuleni ni tatizo linaloendelea kusumbua baadhi ya wanafunzi nchini na kusababisha wakatishe masomo. Jamii ina mchango gani katika kukabiliana na tatizo hilo? Wadau wanajadili.



**VAILETH SHIMWELA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NIANZE kwa kusema kuwa elimu ya makuzi ni ya muhimu sana hasa zama hizi ambazo mmomonyoko wa maadili umekuwa mkubwa.

Watu wana tamaa ya kupata mali na wanasababisha kuendelea kuongezeka kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni na kuwafanya wakose haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Baadhi ya wazazi huwalazimisha watoto wao kuolewa katika umri mdogo na hawatoi ushirikiano pindi tatizo linapotokea pamoja na kuficha wanaohusika na matukio hayo.

Lakini ninaamini wapo wazazi wanaowapa watoto wao elimu ya makuzi ili kuepuka mimba, na hata shuleni na katika makongamano inatolewa, kinachokwamisha ni hilo tatizo la mmomonyoko wa maadili.

Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuona ana jukumu la kuelimisha mtoto wake juu ya mimba hizi. Wazazi ambao wamekuwa wakishirikiana na wahalifu kwa kupokea chochote na wanakwamisha juhudi za kuongeza uelewa wa stadi juu ya masuala ya afya ya uzazi kwa vijana wa kike na kuwafanya wasijikinge na mimba za utotoni wasionewe huruma.

Mimba za utotoni ni hatari, wazazi watenge muda wa kuzungumza na watoto wao, waache visingizio kwamba wana shughuli nyingi.

Kutenga muda kwa ajili ya kutoa elimu ya makuzi kwa watoto ni muhimu sana, kwani dunia ya leo imebadilika.

Kwa ujumla ni kwamba watoto wasaidiwe kwa kila njia kuepuka mazingira yanayoweza kuwaingiza kwenye vishawishi vya kufanya ngono ambavyo mwisho wake siyo mzuri kwao.



**JOHN KILLAWE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

ZAMA hizi siyo za kuona aibu tena kwani watoto wa kisasa wanajua mambo mengi mapema, hivyo wazazi au walezi hawana budi kukaa nao na kuwaambia ukweli kuhusu madhara ya mimba.

Ninatambua kwamba kuna changamoto nyingi zinazochangia mimba za utotoni ukiwamo umaskini wetu, ambao unawafanya watoto washawishiwe kwa kupewa chochote na kujikuta wakishiriki vitendo vya ngono na kupata mimba au maradhi, lakini umaskini huo haumzuii mzazi kukaa na mtoto wake na kumwambia kila kitu. Hata kama atakuwa mgumu kuelewa, ipo siku atakumbuka kwamba alishaonywa. Mimba ni janga kubwa kwani kila kona ya Tanzania utasikia idadi kubwa ya wanafunzi wamekatisha masomo kwa sababu ya mimba.

Inauma sana kuona mtoto akishindwa kutimiza ndoto za maisha yake ya baadaye. Elimu ni moja ya haki za msingi za mtoto. Anapokatisha masomo kwa sababu ya mimba anakosa haki hiyo. Wazazi na walezi watenge muda hata wa nusu mara moja kwa siku kwa kukaa na watoto wao na kutoa elimu juu ya madhara ya mimba hizi za utotoni.

Ninatambua juhudi za walimu jinsi, ambavyo wamekuwa wakijitahidi kuelimisha wanafunzi kwa undani kuhusu mimba na hasa katika la Sayansi, wale wanaozingatia litakuwa linawasaidia kutambua madhara ya kiafya yanayotokana na mimba za utotoni na kuacha kujihusisha na masuala ya ngono katika umri mdogo, ingawa wakati mwingine inawezekana wasizingatie, lakini utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na makuzi ni ya muhimu kuanzia nyumbani, shuleni na hata kwenye jamii kwa ujumla. Pamoja na hayo, Mungu awe ni wa kwanza kwa kila jambo.



**LEONARD MBANGILE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SABABU za tatizo la mimba zinaweza kuwa nyingi. Lakini kubwa kabisa ni umaskini wa kipato ambao unawakabili Watanzania wengi na pia baadhi ya wasichana wanapenda kufanikiwa kwa njia ya mkato ndiyo maana wanajiingiza katika matendo machafu wangali wadogo.

Utaona wanageuza miili yao kuwa kama kitegauchumi na unakuta baadhi ya wazazi wanashirikiana na watoto wao kufanikisha vitendo hivyo kwa kukubali kupokea chochote kutoka kwa wahalifu pale watoto wao wanapopata mimba.

Hata katika vyuo ingawa hawa ni watu wazima, nako kuna tabia chafu, utakuta msichana akimuona mwenzake anaendesha gari, naye lazima atafute mtu wa kumpatia usafiri au akiona mwenzie ana pafyumu nzuri, viatu vizuri au simu nzuri, basi lazima naye atafute mtu au watu watakaompa vitu kama hivyo.

Kwa hiyo utaona kwamba baadhi ya wasichana siyo watu wa kuridhika na hali zao za kawaida ndiyo maana wanajiingiza katika mambo haya.

Swali kwamba  jamii ina sehemu gani katika kukabiliana na mimba, majibu yangu ni kwamba ina sehemu kubwa sana, kwa sababu kuna njia nyingi za kupata elimu huanzia nyumbani na kisha shuleni na hata kwenye vyombo vya habari.

Jamii ina nafasi kubwa kuelimisha na pia kila mtu amuone mtoto wa mwenzake kama wake.



**ALLY SULEYMAN (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HILI jambo linatakiwa kujadili kwa upana wake, kwani hata mimi mwenyewe sijawahi kuwafundisha watoto wangu, ninahofia kwamba unaweza kuwafundisha ndiyo ukawa umewachochea kuingia katika tabia chafu. Ninajua kuwa serikali, mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali na hata shule, elimu hiyo imekuwa ikitolewa.

Maana yangu ni kwamba zipo njia nyingi ambazo mtoto anaweza kupata elimu kuanzia nyumbani kwao. Hata kama mimi siwafundishi wanangu, mama yao anafanya kazi hiyo. Pia kuna matangazo ya fataki yanayoelezea madhara ya kukubali kuingia katika mahusiano mapema. Binafsi ninayapenda ingawa baadhi ya watu wanadai kuwa yanadhalilisha eti kwa vile yanaonyesha kwamba unaweza kumnunulia binti chips, soda na gaguro la mtumba na kumpata kirahisi.

Ni kweli baadhi ya watoto wa kike hupenda kupokea hizo chips na vitu vingine bila kujua na kuingia kwenye mtego, hivyo matangazo ya fataki ni elimu tosha kwao inawafanya wawe makini ili wasinaswe kirahisi katika mtego huo wa kuwaharibia maisha.  Katika kufikisha ujumbe sehemu kuna njia mbalimbali za kutumia ikiwamo hii ya tangazo la fataki, lakini bado wazazi na jamii kwa ujumla ina nafasi ya kusaidia watoto wao ili waweze kufikia malengo ya maisha badala ya kukatishwa kwa kupewa ujauzito.

Wasichana wanatakiwa kuacha kushika mambo mawili kwa wakati mmoja, kwani wahenga walisema mshika mbili, mmoja humponyoka.



**REIDA MBWILO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIDHANI kama kuna mzazi asiyemtakia mema mtoto wake kwa kutompa elimu ya kuepuka mimba.

Kinachotakiwa ni watoto wenyewe kufanyia kazi kile wanachoelekezwa kwa ajili ya manufaa yao kwa kujilinda, kujiepusha na mazingira na tabia hatarishi ikiwamo vishawishi rika kama vile kutoanza mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo, utoro na ulevi.

Kwa kufanya hivyo watajiepusha na mimba za utotoni. Hivyo kila mzazi anatakiwa kuhakikisha anatokomeza tatizo hilo. Vijana hasa wanafunzi ni kundi linalokabiliana na mabadiliko makubwa katika miili yao, ambayo huwaweka katika hatari kubwa ya kukumbwa na matatizo ya kujamiiana na kupata mimba katika umri mdogo, vifo vitokanavyo na uzazi, utoaji mimba na magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya kujamiiana ikiwa ni pamoja na Ukimwi.

Mimba za utotoni zinachangia kuongeza umaskini katika jamii ikiwamo kukosa huduma muhimu, kukosekana kwa wasomi kwani watoto wa kike hushindwa kuendelea na masomo.

Mbali na hayo, mimba za utotoni zinasababisha kuongezeka kwa watoto wa mitaani, kuongezeka kwa vijana tegemezi na kushamiri kwa uhalifu, kuhatarisha maisha ya mama na mtoto wakati wa kujifungua na watoto kukosa baba maalum na malezi bora.



## HABARI MBEYA

# Kaya 200 Mbeya zakosa umeme kwa miezi sita

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

ZAIDI ya kaya 200 katika Kijiji cha Kimondo Kata ya Igoma wilayani Mbeya, zimekosa huduma ya umeme kwa miezi sita kutokana na kuharibika kwa Transfoma tangu mwezi Oktoba mwaka jana.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wananchi hao walisema transfoma hilo liliungua baada ya kupigwa na radi na Shirika la Umeme nchini (Tanesco) halijabadilisha mpaka sasa licha ya kuwaahidi kuwa lingewapelekea mpya.

Mmoja wa wananchi hao, Juma Shaban, alisema kutokana na tatizo hilo, wananchi wamelazimika kurudi kwenye zama za kutumia vibatari na mishumaa.

Vilevile, alisema wananchi wanalazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 15 kwenda kwenye vijiji jirani kwa ajili ya kufuata huduma ya kusaga unga.

"Tunapata tabu sana, matumizi ya mishumaa na vibatari vinahatarisha maisha ya familia zetu, lakini tunakosa mawasiliano ya simu kwa sababu hatuwezi kuchaji simu zetu na shughuli zetu za kiuchumi zinakwama," alisema Shaban.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Suleimain Mbipa, alisema amejaribu kulifuatilia suala hilo katika Tanesco, lakini hakuna majibu mazuri wanayoyapata hali ambayo imewafanya wananchi waanze kuichukia serikali.

Alisema baadhi ya wananchi hao wameanza kuingiza masihara kwenye suala hilo hali ambayo alidai kuwa inaichafua serikali.

"Nimesaidiana na Diwani wa Kata ya Igoma, Fredy Mwankenja, mpaka sasa wananchi wamekata tamaa na baadhi wana hasira na serikali yao," alisema Mbipa.

Ofisa uhusiano na huduma kwa wateja wa Tanesco Mkoa wa Mbeya, Sham Lameck, alisema shirika hilo tayari limeshanunua transfoma mpya kwa ajili ya kwenda kulifunga katika kijiji hicho.

Aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuendelea kuwa wavumilivu wakati Tanesco inaendelea na utaratibu wa kwenda kufunga transfoma hiyo na kwamba watapata umeme wa kutosha.

# Matatani tuhuma mauaji ya mpenzi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia kijana aliyetajwa kwa jina la Festo Maduhu mwenye umri kati ya miaka 28 mpaka 30, mkazi wa Kabwe jijini Mbeya kwa tuhuma za kumuua mpenzi wake.

Maduhu anatuhumiwa kufanya kitendo hicho wakiwa kwenye nyumba ya kulala wageni.

Aidha, kijana huyo anatuhumiwa kujaribu kujiua kwa kujichinja koromeo baada ya kumuua mpenzi wake akikwepa kukamatwa na Polisi wakati akifuatiliwa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulric Matei, alisema tukio hilo lilitokea Machi 22, mwaka huu majira ya saa 3:00 asubuhi ambapo kijana huyo alimuua mpenzi wake, Jesca Michael (28).

Kamanda Matei alisema kijana huyo aliimuua mpenzi wake huyo kwa kumkaba shingo na kumshushia makonde sehemu mbalimbali za mwili ikiwamo usoni wakiwa ndani ya moja ya chumba cha kulala wageni ijulikanayo kwa jina la Negero, ambayo mwanamke huyo alikuwa anafanyia kazi kama mhudumu.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa mapenzi kwa maelezo kuwa maelezo kuwa Maduhu alikuwa anamtuhumu mpenzi wake huyo kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanamme mwingine, ambaye jina lake limehifadhiwa.

"Mtuhumiwa alikutwa amejifungia nyumbani kwake na baada ya askari kuvunja mlango wa nyumba hiyo, alikutwa anaendelea kujichinja koromeo na askari walimwokoa na kumpeleka katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa ajili ya matibabu," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei alisema mwili wa Jesca umehifadhiwa katika hospitali hiyo, na mtuhumiwa anaendele kutibiwa akiwa chini ya ulinzi wa Polisi.

Alisema baada ya kupatiwa matibabu hayo na kupata nafuu atahojiwa na Polisi kisha atafikishwa mahakamani.



Baadhi ya wasafiri kutoka Mkoa wa Mbeya kuelekea Tabora na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Chunya, wakivuka kwa miguu katika daraja la Mto Lupa, mwishoni mwa wiki, baada ya mkuu wa wilaya hiyo, kuzuia magari kuvuka kutokana na kipande kimoja cha daraja hilo kuvunjika na kusombwa na mafuriko. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wamiliki wa mabasi wakaidi waonywa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI mkoani Mbeya imetangaza kuchukua hatua kali kwa wamiliki wa magari ya abiria yanayoanzia safari zake mkoani humo kwenda katika mikoa mingine ambao hawataandaa maji na sabuni kwa ajili ya abiria kunawa.

Hatua hiyo ni moja ya tahadhari dhidi ya kusambaa kwa virusi hatari vya corona.

Hatua hiyo ilitangazwa jana katika Kituo Kikuu cha mabasi cha jijini Mbeya na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alipofanya ziara ya kushtukiza kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa agizo hilo ambapo alisema basi lolote ambalo litakuwa halina maji na sabuni litazuiwa kuendelea na safari.

Alisema kutokana na mlipuko wa homa hiyo ya corona, kila abiria anayepanda kwenye basi kwa ajili ya kuanza safari ni lazima anawe mikono kwa majisafi na sabuni ili kuepuka kujikinga na virusi hivyo, na kwamba wamiliki wa mabasi wanatakiwa kuwaelekeza madereva wao.

Ntinika alisema katika Mkoa wa Mbeya hakijatokea kisa chochote cha mtu kuambukizwa ugonjwa huo, hivyo akawataka wananchi kuendelea kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

"Lakini mbali na hizi hatua, nawaomba wananchi ambao hawana sababu za kusafiri wabaki nyumbani maana huu ugonjwa ni hatari sana, tujitahidi sana kupeana elimu sahihi ili kuuepuka," alisema Ntinika.

Alisema ufuatiliaji wa uwapo wa maji na sabuni kwenye mabasi utaendelea kwa muda wa mwezi mzima na kwamba ikiwezekana muda huo utaongezwa ili kuhakikisha wananchi wanakuwa salama.

Alisema serikali kupitia wataalamu wake itaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kujikinga na janga hilo la dunia ili kuhakikisha linadhibitiwa ipasavyo.

Vilevile, alisema ufuatiliaji wa mabasi utafanyika kila siku kwenye vituo vyote vya mabasi na kwamba madereva na makondakta wa mabasi watakaoshindwa kufuata taratibu hizo watachukuliwa hatua kali.

Mganga Mkuu wa Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala, ambaye aliambatana na Mkuu wa Wilaya, alisema wananchi wa Mkoa wa Mbeya waliipokea elimu hiyo vizuri na wanaendelea kufuata taratibu zilizoelekezwa.

Alisema katika zoezi hilo walibaini mabasi yote yalikuwa na maji pamoja na sabuni, kwamba hakuna abiria hata mmoja ambaye alibainika kugoma kunawa mikono kwa sababu yoyote.

Alisema mbali na maji kuwamo kwenye mabasi, lakini kila ofisi ya kukatia tiketi ina maji na sabuni kwa ajili ya abiria wanaoenda kukata tiketi na hivyo kuna uwezekano kuwa elimu imewaingia vizuri wananchi hao.

"Tumeongea pia na abiria wa mabasi kwa ajili ya kujua kama wana uelewa wa kutosha kuhusu janga hili na wamethibitishia kuwa wanaelewa maana hata maoni waliyotupatia ni mazuri sana," alisema Dk. Lulandala.

Kadhalika, aliwataka wakazi wa Jiji la Mbeya kuendelea kufuata masharti hata nyumbani badala ya kuishia kuyafuata kwenye maeneo ya umma ambayo yamepewa maelekezo maalumu.

Aliwataka pia wananchi kuacha mizaha kwenye ugonjwa huo ikiwemo kusambaza taarifa za uongo kuhusu ugonjwa huo hatari ambao unatesa dunia kwa sasa.

Baadhi ya abiria waliishukuru serikali kwa hatua ambazo inaendelea kuzichukua juu ya kukabiliana na janga hilo kwa maelezo kuwa zitasaidia kuwakinga wananchi.





# Jiji la Dodoma latakiwa kudhibiti ujenzi holela

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameitaka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kudhibiti ujenzi holela ili kuwa na Jiji lililopangwa.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika hafla ya kukabidhi magari matatu kwa ajili ya kitengo cha udhibiti wa ujenzi holela kilicho chini ya Idara ya Ardhi, Mipango miji na Rasilimali kwenye jiji hilo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi magari hayo, mkuu huyo alisema mkoa hautegemei kutakuwapo na ujenzi holela na kulitaka jiji hilo kudhibiti hali hiyo kutokana na kukua kwa kasi na ujenzi kushamiri kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema uwapo wa vitendea kazi mahsusi kwa ajili ya ukaguzi wa maeneo yanayofanywa ujenzi holela utasaidia kudhibiti hali hiyo.

"Naamini hakutakuwa na ujenzi wa aina hiyo maana watendaji watapita mapema na kudhibiti ujenzi kabla mwananchi hajafika hatua ya kukamilisha ujenzi huo na maeneo ambayo hayana mpangilio, niwaombee mtumie vitendea kazi hivyo kwa jukumu lililokusudiwa na si kubebea magunia ya mkaa au kufanyia kazi binafsi," alisema Dk. Mahenge.

Aliwaonya wananchi wanaofanya ujenzi kwenye maeneo ambayo yamehifadhiwa ikiwamo maeneo ya wazi na maeneo ya milima.

Aliwataka wananchi kuzingatia taratibu za ujenzi zinazotolewa na jiji na watakaokaidi atatoa kibali cha kuwabomolea.

Awali, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema alisema magari hayo, yamegharimu Sh. milioni 345 ambazo ni mapato ya ndani ili kuimarisha kitengo hicho.

Kunambi alisema jiji limeamua kuimarisha kitengo cha udhibiti wa ujenzi holela kwa kununua vitendea kazi hivyo ili kurahisisha utendaji kazi kwenye idara hiyo.

Alisema lengo ni kuendelea kupima kwa haraka maeneo yanayokua kwa kasi ili kusiwe na ujenzi holela.

**"Naamini hakutakuwa na ujenzi wa aina hiyo maana watendaji watapita mapema na kudhibiti ujenzi kabla mwananchi hajafika hatua ya kukamilisha ujenzi huo na maeneo ambayo hayana mpangilio, niwaombee mtumie vitendea kazi hivyo kwa jukumu lililokusudiwa na si kubebea magunia ya mkaa au kufanyia kazi binafsi," alisema Dk. Mahenge.**

# Vijana zaidi ya 2,000 wapata ujuzi

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

OFISI ya Waziri Mkuu kupitia programu ya kukuza ujuzi imewapatia mafunzo vijana 2,260 kati yao 1,240 tayari wamepata ajira.

Programu hiyo inatekelezwa na Taasisi ya Don Bosco Net Tanzania ili vijana wawe na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na kuongeza wigo mpana wa kujiajiri au kuajiriwa.

Akizungumza jana kuhusu programu hiyo, Mkuu wa Chuo cha Don Bosco, Padri Boniface Mchami, alisema vijana hao waliopata ajira ni sawa na asilimia 50 ya waliopata ujuzi.

Alisema fani zitakazofundishwa kupitia programu hiyo ni kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji, ufundi bomba, useremala, uchomeleaji vyuma, uchongaji wa vipuri vya mitambo, uashi, uwekaji wa terazo na vigae kwenye majengo.

Pia alisema wamefundishwa ufundi magari na mitambo, kilimo na ufugaji, kutengeneza kompyuta, kuchapa vitabu na nyaraka, pamoja na kufunga umeme ukiwamo wa mwanga wa jua (solar) wa majumbani na viwandani.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha vijana hao wanajiajiri au kuajiriwa ili kuongeza nguvu kazi ya taifa.

Alisema taifa linahitaji kufika katika uchumi wa viwanda hivyo ni vema vijana wasome ili kufikia malengo ya taifa.

Alifafanua kuwa vijana wengi ambao wamepitia mafunzo hayo wametambua thamani ya ufundi stadi na kuwaasa wengine wasibweteke badala yake wasomee ufundi huo.

Alitoa wito kwa watoto wa kike kwenda kusomea ufundi stadi na kuacha kuchagua kazi.

Naye Mwanafunzi Naftari Mazengo aliishukuru serikali kwa elimu hiyo na kuwahimiza wengine kuchangamkia fursa.

Happiness Jackson, alisema masomo hayo yamempa manufaa makubwa na kuwaasa wasichana kutokubali kubaki nyuma kiujuzi.



Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la EAGT, lililopo Ipagala, jijii Dodoma, Lucas Evance (katikati), akiwaongoza waumini wa kanisa hilo kunawa maji na sabuni, kabla ya kuingia ibadani ili kujilinda na maambukizi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC ataka ukarabati wa dharura daraja Idilo

**Na Mwandishi Wetu, MPWAPWA**

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma Jabir Shekimweri, ameutaka Wakala wa Barabara Nchini (Tanroads), kufanya ukarabati wa dharura kwenye daraja la Idilo lililoharibiwa na mvua ili kujiepusha kukatika mawasiliano wilayani humo.


Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki alipofanya ziara akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya kwenye daraja hilo ili kuangalia athari zilizosababishwa na mvua.

Shekimweri alisema, kamati hiyo inafanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kujiridhisha na kushauriana na Tanroads na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura), kuhusu hatua za kuchukua.

"Mvua kubwa iliyonyesha imeleta uharibifu katika miundombinu ya barabara, kama tunavyoona barabara za kiwango cha changarawe zimeathirika sana na zinapitika kwa tabu hivyo tayari mkandarasi ameteuliwa ili aanze kazi," alisema Shekimweri.

Hata hivyo, alisema kuna uharibifu mkubwa kwenye madaraja na makaravati huku matengenezo yakikumbwa na adha ya mvua zinazoendelea kunyesha na kushauri ni vyema matengenezo madogo yafanyike kwa sasa wakati wakisubiri mvua iishe au kupungua.

Alihimiza Tarura na Tanroads kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa madaraja na makalvati hususani wakati wa mvua na kuchukua tahadhari mapema kabla ya athari kubwa kutokea.



# Wizara: Kuna wagonjwa wengi TB hawajabainika

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Afya Zanzibar, imesema bado kuna idadi kubwa ya wagonjwa wa kifua kikuu ambao hawafiki vituo vya afya na kugundulika mapema, au hata wakifika katika vituo vya afya bado hawagunduliwi na kuanza matibabu mapema.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani, Waziri wa Afya, Hamad Rashind Muhammed, alisema kulingana na ripoti ya Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), kifua kikuu ni kati ya magonjwa 10 yanaoongoza kwa vifo ulimwenguni na ni ugonjwa unaoongoza kwa kusababisha vifo katika ya maradhi yanayoambukiza ulimwenguni.

Alisema licha ya jitihada zinazochukuliwa, bado kuna idadi kubwa ya wagonjwa wa kifua kikuu ambao hawajajitokeza na kupata tiba sahihi, na hivyo kuendeleza maambukizo katika jamii.

Alisema katika mwaka 2018, watu milioni 10 waliugua ugonjwa huo duniani. Kati yao, milioni 1.5 walikufa kutokana na maradhi hayo, sawa na wastani wa watu 4,100 kwa siku.

Alisema kwa Tanzania ni kati ya nchi 30 ulimwenguni zenye idadi kubwa ya wagonjwa wa kifua kikuu, akibainisha kuwa kwa mwaka 2018, wagonjwa wapatao 75,845 waliripotiwa kuugua ugonjwa huo, ikiwa ni ongezeko kutoka wagonjwa 69,819 wa mwaka 2017.

Alisema kwa upande wa Zanzibar, wastani wa wagonjwa wapatao 700 hadi 900 wanagundulika kuwa na maradhi hayo kila mwaka.

"Katika mwaka 2019, wagonjwa 967 waligundulika na maradhi hayo ikiwa ni ongezeko kutoka wagonjwa 944 wa mwaka 2018, japokuwa idadi hii inaonekana ni kubwa, lakini bado ipo chini ya makadirio ya wagonjwa 1,600 wanaokadiriwa kuugua maradhi hayo kila mwaka hapa kwetu," alisema.

Aliongeza kuwa Zanzibar bado kuna uelewa mdogo katika jamii juu ya dalili za ugonjwa huo, hivyo wananchi huchelewa kufika katika vituo vya afya.

"Ili kutokomeza kabisa maradhi haya, ni lazima tuwagundue na kuwatibu wale wote ambao wana ugonjwa huu," alisema.

Waziri huyo aliwataka wananchi wote hufahamu kwamba wana wajibu wa kufika katika vituo vya afya mara tu baada ya kuonyesha dalili za maradhi hayo.

Alisema kuchukua hatua dhidi ya tatizo la kifua kikuu duniani, Bara la Afrika, Tanzania na Zanzibar ni muhimu kutokana na ongezeko kubwa la maambukizo ya ugonjwa huo.

"Kifua kikuu ni moja ya maradhi ya kuambukiza ambayo huua watu kwa wingi sana," alisema.

Meneja Msaidizi wa Programu ya Kifua Kikuu, Homa ya Ini na Ukimwi, Issa Abedi Mussa, alisema huduma za matibabu ya kifua kikuu zimeimarishwa kwenye vituo vyote mijini na vijijini.




Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Muhammed, akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, kuhusu Siku ya Kifua Kikuu, itakayoadhimishwa leo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Shein apongezwa kwa Sheria Mfuko wa Pensheni

**Na Mwandishi Wetu, UNGUJA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimempongeza Rais Ali Mohamed Shein kwa kuanzisha Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Jamii kwa wazee wenye umri wa kuanzia miaka 70 wakipewa Sh. 20,000 kwa mwezi, kikisema atakakumbwa kwa kuacha alama hiyo muhimu.

Pongezi hizo zilitolewa na Katibu wa Kamati Maalum ya Itikadi na Uenezi ya CCM Zanzibar, Catherine Peter Nao, alipozungumzia miaka tisa ya uongozi wa Rais Shein tangu aingie madarakani mwaka 2010.

Catherine alisema Rais Shein katika utekelezaji wa majukumu yake ya kimsingi, kisera na kiutendaji, ametimiza kwa vitendo mpango wa kuwajali wazee na kuwalipa Sh. 20,000 kwa mwezi kama pensheni na kujenga kumbukumbu ya mnara wa Mapinduzi Matukufu.

Alisema Rais Shein amekuwa akipita juu ya nyayo za Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume kwa kujali wazee na kuwatunza kwenye makazi maalum, kuendeleza sera ya elimu bure, kuanzisha miradi ya maji na makazi bora ya kisasa.

"Sera ya kuwatunza wazee ni ya ASP ikiendelezwa sasa na CCM chini ya Rais Shein. Rais ameona jambo hilo liwe la kudumu, serikali sasa imeunda sheria ya kuwalipa wazee kila mwezi. Ni mkakati wa kuboresha afya ya jamii kwa wazee hao kupatiwa chakula katika nyumba wanazoishi," alisema.

Aliongeza kuwa Mzee Karume alianzisha sera ya kuwahifadhi wazee wasiojiweza, serikali yake ikajenga nyumba za kutunza wazee na sasa Rais Shein ameona ipo haja ya kuanzisha Sheria ya Mfuko wa Pensheni ya Jamii kwa Wazee.

Alisema nyumba za kuhifadhi wazee Zanzibar zimefanyiwa matengenezo makubwa pamoja na kutoa huduma nzuri za milo mitatu kwa siku na kuimarisha huduma za afya ili kuwapa faraja na kuwajali wazee.

Alisema uongozi wa Rais Shein una mambo mengi ya kujivunia yalioanzishwa katika sekta ya elimu, afya, miundombinu ya barabara, utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia unaoendelea visiwani.

"Serikali ya awamu ya saba imenunua meli ya abiria, mizigo na ya mafuta. Tunatarajia hasara ya watu kuzama baharini itabaki historia. Tuna meli mpya ya abiria iitwayo Mapinduzi na meli ya mafuta. Imeanzishwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (Zafico) na kununua meli ya uvuvi wa bahari kuu imefika moja kati ya mbili," alitamba.

# 'Unyanyapaa unachangia maambukizo mapya VVU'

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

KUENDELEA kwa unyanyapaa katika jamii dhidi ya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU), kunachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa maambukizo mapya visiwani Zanzibar.

Ofisa Habari, Mawasiliano na Uhamasishaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar (ZAC), Sihaba Saadat Haji, aliyasema hayo katika kikao kazi na waandishi wa habari kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Studio Rahaleo.

Alisema wapo baadhi ya watu wanashindwa kujitokeza kuzungumzia hali zao kwa kuhofia kunyanyapaliwa katika maeneo yanayowazunguka hasa kwenye familia na sehemu za kazi.

Alisema hali ya unyanyapaa kwa Zanzibar ni zaidi ya asilimia 23.4 na kwamba maeneo ya vijijini upo juu zaidi kulinganisha na maeneo ya mjini hasa kisiwani Pemba ambao upo kwa asilimia 38.

Ofisa Saadat alisema mikoa inayoongoza kwa unyanyapaa huo ni Kaskazini Pemba asilimia 45.4, Kusini Pemba asilimia 32.4, Kaskazini Unguja asilimia 29.4, Kusini Unguja 19.3 na Mjini Magharibi asilimia 16.6.

Alisema unyanyapaa unatokea katika sehemu mbalimbali, lakini maeneo yanayoongoza kwa unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU ni maeneo ya kazi, tiba na ibada.

Akizungumzia athari za unyanyapaa katika jamii, ofisa huyo alizitaja kuwa ni pamoja na mzazi, kujenga hofu ya kupima, hivyo hupelekea kuongezeka kwa maambukizo mapya, mtoto kukosa huduma stahiki kutokana na hofu ya mzazi kujulikana na jamii, watoto hudumaa na kukosa kukua vizuri kimwili na kiakili, kukosa fursa ya kucheza na kuchanganyika na wenzao na baadaye hufariki dunia.

Ofisa huyo alisema kuna umuhimu mkubwa wa kupunguza hali ya unyanyapaa ili kupunguza kasi ya kuenea kwa VVU, watu watajitokeza kupima afya zao, kurahisisha uwazi na mmoja kumweleza mwenza wake hali yake ya maambukizo, kuondoa tatizo la kuvunjika kwa ndoa kusiko kwa lazima na kupunguza vifo vinavyotokana na Ukimwi.

Sambamba na hayo, alisema bado elimu inahitajika zaidi kwa jamii kuacha kuwanyanyapaa watu wanaoishi na VVU ili kufikia lengo la kutokomeza ugonjwa huo kwa kupunguza maambukizio mapya.

Mratibu kutoka Mradi wa Afya Kamilifu (AMREF), Sandey Bebwa, alisema kwa kushirikiana na ZAC, wanaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuondoa unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU na kuleta mabadiliko ndani ya jamii.

Alisema vikwazo vilivyopo ni uwelewa mdogo kwa jamii kuhusu unyanyapaa, hivyo wataendelea kuchukua hatua zinazofaa ikiwamo kuendelea kuelimisha jamii ili kuondokana na dhana hiyo potofu.

# Wakulima wa Handeni, Korogwe wahofia mvua

**Na Boniface Gideon, HANDENI**

WAKULIMA wa Wilaya za Handeni na Korogwe mkoani Tanga wapo katika wakati mgumu kutokana na kupanda mazao, huku wakikosa mvua za uhakika.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakulima hao walisema wapanda mazao wiki mbili zilizopita, lakini mpaka sasa hakuna mvua, huku mazao yakianza kunyauka.

Abdallah Salehe, mkazi wa Kata ya Kwamatuku wilayani Handeni, alisema wamepanda mazao hususani mahindi, lakini yameota kwa kusuasua.

"Tumepanda mahindi, lakini mengi hayajaota kwa kukosa mvua, lakini hatujakata tamaa kwa kuwa bado tunaendelea kuisubiri mvua mpaka mwisho wa mwezi huu," aliongeza Salehe.

Naye Zainabu Yahaya, alisema mpaka sasa bado wanaendelea kusubiri kama mvua zitanyesha. "Hatuna matumaini maana mvua za vuli zimenyesha sana, na tumevuna mahindi mengi, lakini safari hii sijui kama tutafanikiwa," alisema Zainabu.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Handani Vijijini, Mustafa Beleko ambaye ni Diwani wa Kata ya Kwamatuku, alikiri kutokunyesha kwa mvua.

"Nikweli mvua hazijaanza na kuna wakulima wamepanda mazao na wengine bado wanaendelea kuandaa mashamba, lakini bado tunaendelea kusubiri maana hizi ndio tarehe zenyewe," alieleza diwani Beleko.

Beleko alisema kuna baadhi ya wakulima walipanda mazao wiki kadhaa zilizopita baada ya mvua kunyesha, lakini mvua haijarudi tena, hali iliyofanya baadhi ya maeneo mahindi kushindwa kuota inavyopaswa, hivyo kuwataka wakulima kuendelea kuandaa mashamba kwa kuwa mvua zipo.

**"Nikweli mvua hazijaanza na kuna wakulima wamepanda mazao na wengine bado wanaendelea kuandaa mashamba, lakini bado tunaendelea kusubiri maana hizi ndio tarehe zenyewe," alieleza diwani Beleko.**

# Tume yawachunguza wahandisi aliowasimamisha kazi Magufuli

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi), Elius Mwakalinga, ameunda tume iliyoanza kufanya uchunguzi kwa wahandisi 12 wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Morogoro ili kubaini endapo kulikuwa na uzembe na hujuma baada ya daraja la Kiyegeya kukatika.

Daraja hilo lipo wilayani Kilosa katika barabara kuu ya Morogoro- Dodoma, ambalo lilikatika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Tume hiyo ambayo imeanza kufanya kazi iliyopewa siku saba kukamilisha uchunguzi huo, pia ina jukumu la kujua athari za kiuchumi zilizopatikana kwa kipindi cha daraja hilo lilipokatika na magari kushindwa kupita kwa siku tatu.

Kuundwa kwa tume hiyo kumetokana na agizo la Rais John Magufuli alipotembelea daraja hilo na kubaini kuwapo kwa uzembe kwa watendaji na wahandisi wa mkoa huo na kuamua kuwasimamisha kazi, hivyo kumuagiza Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Isack Kamwelwe, kuunda kamati ya kuwachunguza.

Akizungumza na waandishi wa habari, baada ya uzinduzi wa magari kupita katika daraja hilo katika barabara ya mchepuko, Mwakalinga, alisema tume hiyo imeshirikisha wataalamu kutoka nje ya Tanroads.

"Tume hiyo tayari imeshaanza kazi na imepewa siku saba ili kukamilisha uchunguzi huo," alisema Katibu Mkuu huyo.

Aliwataja wataalamu waliopo katika tume hiyo ni wahandisi na wauchumi, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB).

Alisema tume hiyo itafanya kazi kwenye eneo la daraja la Kiyegeya na ofisi zake kwa muda itakuwa katika chuo cha ujenzi cha mjini Morogoro.

Naye Waziri Kamwelwe, alisema tumetekeleza maagizo yaliyotolewa na Rais Dk. Magufuli ya kuwasimamisha kazi wahandisi 12 na nafasi zao zimejazwa na watu wengine, ikiwamo kuteuliwa kwa Meneja wa Tanroads mkoa wa Morogoro, Mhandisi Ntije Nkolante, akitokea Mkoa wa Kilimajnaro.

Alisema nafasi ya meneja aliyehamishiwa Mkoa wa Morogoro imezibwa na Mhandisi Motta Kyando ambaye alikuwa Mkuu wa Idara ya Mipango Tanroads Mkoa wa Iringa.

"Kwa hiyo maelekezo ya Waziri Mkuu na Rais kwanza kwa stafu 12 kuwaondoa tumetekeleza na tume tumeunda na siku saba za kukamilisha daraja la mchepuko... tayari limekamilika na magari yanapita muda wote kwa hiyo wasafirishaji wasiwe na wasiwasi tena," alisema Waziri Kamwelwe.

Mhandisi Nkolante alisema anafahamu mkoa huo una changamoto nyingi, lakini amejiandaa kukabiliana nazo kwa kushirikiana na timu mpya ya wahandisi 12 iliyoletwa hivi karibuni.

"Waziri amesema timu nzima imekamilika, hivyo tunaanza kujipanga wote kwa pamoja ili kumaliza changamoto zilizopo na zitakazojitokeza," alisema Mhandisi Nkolante.

Daraja la Kiyegeya lilibomoka Machi 2, mwaka huu kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini na kukata mawasiliano ya mkoa ya Dar es Salaam - Dodoma, Kanda ya Kati, Magharibi, ziwa na nchi jirani za maziwa makuu na kurudishwa mawasiliano Machi 4, mwaka huu kwa kutumia barabara ya muda ya mchepuko na ujenzi wa karavati la muda barabara kuu.



Mtendaji wa Kijiji cha Etaro, Musoma Vijijini, mkoani Mara, Sophia Charles (kulia) na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Etaro, Mangire Mahombwe, wakikagua maendeleo ya ujenzi wa madarasa manne mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wawakilishi waridhishwa uchimbaji mchanga

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa imeridhishwa na udhibiti wa eneo la uchimbaji wa mchanga lililopo Kishindeni Wilaya ya Wete kisiwani Pemba kwa kutoathirika licha ya uchimbaji huo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Panya Ali Abdallah, alisema kuwa, amefurahishwa kuona eneo hilo lililochimbwa mchanga halijaathirika, kutokana na wasimamizi kujitahidi kuweka hadhari mapema kwa usalama wa wananchi.

Aliyasema hayo wakati akikagua eneo la uchimbaji wa mchanga Kishendeni katika ziara ya kamati hiyo ya siku mbili kisiwani Pemba.

Alisema ni jambo zuri na la faraja walilofanya Idara ya Mazingira katika kuhakikisha maeneo yanayochimbwa mchanga hayaathiriwi.

"Kwa kweli eneo lipo vizuri sana, nimeshangaa kuambiwa hapa panachimbwa mchanga... limenifurahisha kwani hata hujui kama pameshawahi kuchimbwa mchanga, wamefuata utaratibu mzuri na eneo litaweza kutumika kwa shughuli za kilimo," alisema Mwenyekiti huyo.

Mwenyekiti huyo aliipongeza Idara ya Mazingira Pemba kwa kuchukua hatua ya udhibiti wa eneo hilo mapema, na kuwataka kuendelea kuangalia maeneo mengine wanayotoa vibali, ili kuyadhibiti yasilete athari.

Mapema akizungumza wakati kamati ilipotembelea nyumba mpya ya kurekebisha tabia (Sober House) Limbani Wete, mwenyekiti huyo alisifu ushirikiano mkubwa wanayopewa na majirani na kumtaka kiongozi wa nyumba hiyo kuzidi kuwanasihi waathiriwa wa dawa za kulevya, ili wakitoka hapo wasirudie kuzitumia.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kheriyangu Mgeni Khamis, alisema haikuwa kazi rahisi kuirejesha Sober House, lakini serikali imefanya jitihada kubwa ili kuhakikisha inaokoa maisha ya vijana nchini.

Akisoma risala mbele ya kamati hiyo, kiongozi wa nyumba hiyo, Thani Salum Said, aliishukuru kamati kwa kuishawishi serikali na kufungua tena nyumba hiyo, jambo ambalo limewapa faraja kubwa, kwani walipokea vijana 40 ambapo vijana saba kati yao wameshaacha kabisa kutumia dawa za kulevya na wanaendelea na shughuli zao za kujitafutia riziki.

# HABARI KIMATAIFA

## Waliofariki kwa corona duniani wafikia 14,300

**ROME,** Italia

WAKATI nchi mbalimbali duniani zikihangaika kupata tiba ama kinga ya ugonjwa wa virusi vya corona, imeelezwa kuwa idadi ya vifo vinavyotokana na mlipuko wa ugonjwa huo imeongezeka na kufikia 14,300 huku 320,000 wakiambukizwa.

Takwimu hizo zilizotolewa jana zilieleza pia nchini Italia takribani watu 60,000 wamepata maambukizi huku idadi ya vifo ikikaribia 5,500.

Nchini Hispania serikali imetangaza kurefusha muda wa hali ya dharura kuanzia jana baada ya idadi ya vifo na maambukizi kuongezeka.

Nchini Misri, Rais Abdel-Fattah el Sissi aliwahimiza raia wake kusaidia kudhibiti kusambaa kwa virusi hivyo kwa kubaki nyumbani na kuepuka kukaribiana wakati nchi hiyo ikithibitisha visa 327 vya maambukizi na vifo 15.

Wakati huo huo, mashirika ya ndege ya Emirates na Turkish Airlines yamesitisha safari zake za kimataifa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona. **DW**

## Taliban, Afghanistan wajadili kuachiwa wafungwa

**KABUL,** Afghanistan

MAOFISA Afghanistan wamesema kundi la Taliban na serikali ya nchi hiyo wamefanya mkutano kwa njia ya video kuhusu kuachiwa kwa wafungwa na kutoa matumaini ya mwafaka juu ya suala hilo.

Pande hizo mbili zimetofautiana kuhusu kuachiwa kwa wafungwa hao na kwamba serikali inataka kuwaachia kwa awamu, huku Taliban ikitaka wafungwa wote kuachiwa mara moja kama ilivyoafikiwa katika makubaliano na Marekani mjini Doha mwezi uliopita.

Mkwamo huo umetishia kurejesha nyuma mchakato wa amani uliojadiliwa kwa umakini kama ilivyoainishwa katika makubaliano hayo yanayojumuisha kuondolewa kwa vikosi vya kijeshi vya kigeni kutoka Afghanistan baada ya zaidi ya miaka 18 ya mapigano.

Mjumbe maalumu wa Marekani nchini Afghanistan, Zalmay Khalilzad, alisema kuwa pande hizo mbili zilizungumza kwa zaidi ya saa mbili kupitia mtandao wa Skype katika mkutano uliowezeshwa na Marekani na Qatar.

Khalizad alisema kila mtu anafahamu kwamba tishio la virusi vya ugonjwa wa corona linafanya suala hilo la wafungwa kuwa la dharura na kwamba pande hizo mbili zilielezea dhamira yao katika kupunguza ghasia, kufanya mazungumzo ndani ya Afghanistan na makubaliano makhsusi ya kusitisha kabisa mashambulizi. **DW**

# Angela Merkel apata corona, ajiweka karantini

**BERLIN,** Ujerumani

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merkel amejitangaza kuathirika na ugonjwa wa virusi vya corona baada ya kupimwa na daktari wake.

Mbali na kijitangaza, Merkel alilihutubia taifa na kutangaza mikakati mipya ya kupambana na ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku ya mikusanyiko ya watu zaidi ya wawili.

**Baadhi ya marufuku zilizotolewa ni kufungwa kwa migahawa na huduma kama vile za ususi.**

Hata hivyo, alisema marufuku hiyo haihusishi familia ama watu wanaoishi pamoja.

Baadhi ya marufuku zilizotolewa ni kufungwa kwa migahawa na huduma kama vile za ususi.

Kwa upande wa umma, Merkel alisema watu wasioishi pamoja wanapaswa kutosogeleana kwa umbali wa mita 1.50 kati yao, Kampuni kufuata kanuni za usafi kwa wafanyakazi, kusafiri kwenda kazini, kusaidia wengine na mazoezi ya kibinafsi bado inaruhusiwa.

Baada ya kutangaza sheria hizo mpya, Merkel aliufahamisha umma kuwa daktari aliyekutana naye siku ya Ijumaa alimpima na kugundulika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona na kwamba atalazimika kuwa chini ya karantini.

Merkel alisema sheria hizo zitatumika kwanza kwa muda wa wiki mbili na kuonya kwamba hatua hizo mpya siyo mapendekezo bali ni sheria na kwamba polisi itasaidia kuhakikisha zinadumishwa. **DW**



Mwanamke kikongwe (95), Alma Clara Corsini raia wa Italia akiwa na madaktari baada ya kutibiwa na kupona ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

# Watu 10 wauawa vurugu za uchaguzi

**CONAKRY,** Guinea

MACHAFUKO yaliyoibuka wakati wa kura ya maoni ya katiba na uchaguzi wa wabunge yaliyofanyika juzi yamegharimu maisha ya watu na wengine wengi kujeruhiwa nchini Guinea.

Vyama vya upinzani ambavyo vilisusia zoezi hilo ambalo lilipingwa na jumuiya ya kimataifa unakusudia kuzuia muhula wa tatu wa Rais Alpha Condé.

Watu 10 ndiyo waliuawa katika machafuko hayo, kwa mujibu wa vuguvugu linalodai kulinda katiba ya nchi (FNDC) kwa siku moja tu ya Jumapili.

Hata hivyo, Wizara ya Usalama nchini humo imebaini kwamba watu wanne ndiyo waliuawa kwa siku ya jana ikiwa ni pamoja na wawili katika ghasia, mmoja kwa ajali na mwengine kwa mshtuko wa moyo, bila maelezo zaidi.

Taarifa hiyo ya Wizara ya Usalama imeongeza kuwa maofisa tisa kutoka kitengo maalumu cha usalama wa uchaguzi, pamoja na maofisa saba wa polisi, walijeruhiwa vibaya, wakati (FNDC) likitangaza kwamba wafuasi wake kadhaa wamejeruhiwa kwa risasi.

Ilieleza kuwa waandamanaji walishambulia vituo vya kupigia kura, waliharibu na kuchoma vifaa vya uchaguzi katika miji kadhaa nchini na katika maeneo ya mji wa Conakry yenye wafuasi wengi wa upinzani.

Watu kadhaa wamekamatwa kwa makosa ya kuhusika katika machafuko hayo na kuhatarisha usalama wa raia, kumiliki na kutumia silaha za moto kinyume cha sheria.

Makosa mengine ni uharibifu wa mali ya umma, kuchoma moto vifaa vya uchaguzi, kupiga na kufanya uasi dhidi ya serikali.

Hayo yanajiri wakati vuguvugu la FNDC limetoa wito kwa wafuasi wake kuendelea na maandamano. **RFI**

## Wahalifu ubakaji, mauaji wanyongwa

**NEWDELH,** India

WATU wanne wamenyongwa baada ya kupatikana na hatia ya makosa ya ubakaji pamoja na mauaji ya mwanafunzi wa miaka 23 mjini New Delhi.

Kesi hiyo ilianza kumulika vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wanawake nchini India. Wanawake katika mji huo mkuu wa India, wametaja kuwa ni moja ya miji isiyokuwa salama duniani, na hali bado haijatengemaa.

Maandamano kufuatia kitendo hicho cha kinyama cha ubakaji wa mwanamke mwenye umri wa miaka 23 katika mji mkuu wa India mwaka 2012 ndani ya basi kumetoa shinikizo kuwapo ulinzi zaidi kwa wanawake.

Meneja wa Kampuni ya Kusambaza Chakula, Aastha Sharma, anasema: "Bado tunasikia matukio kama hayo (ya ubakaji) kila wiki, kila mwezi, na kila mwaka. Haikubaliki. Takriban kila siku, kuna tukio la habari zinazoongelea ubakaji mpya. Sidhani kama kuna mabadiliko hata kidogo."

Alisema kutokana na hofu ya kutokuwapo kwa usalama barabarani, wanawake lazima wawe makini wanaposafiri, hususani wakati wa usiku. Alisema wanawake katika mji wa New Delh wanapaswa kuhakikisha hakuna gari, pikipiki, wala hakuna kitu chochote kinachowafuata wakati wakitembea hususani nyakati za usiku. **VOA**



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Biashara ya DCB, Rahma Ngassa (kushoto), wakati wa maonyesho ya Wiki ya Ubunifu yaliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Wa (pili kushoto) ni Kiongozi wa Timu ya Mauzo wa DCB, Fauzia Bairu na Mkurugenzi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Prof. Maulilio Kipanyula. **NA MPIGAPIGA WETU**

## Pikipiki kutumika kudhibiti corona

**Na Jumbe Ismailly,** IRAMBA

WILAYA ya Iramba,mkoani Singida imekabidhi pikipiki kwa maofisa tarafa na kuwataka kuzunguka kwenye maeneo yao kuhakikisha agizo la kupiga marufuku vilabu vya pombe za asili linatekelezwa.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Emanuel Luhahula, alitoa maelekezo hayo kwenye hafla ya kukabidhi pikipiki kwa maofisa tarafa za Kinampanda, Kisiriri, Shelui na Ndago.

Alisisitiza kwamba kutokana na kuwapo kampeni ya kulitokomeza janga hilo, ni jukumu la maofisa tarafa hao kuhakikisha wanazitumia pikipiki hizo kwa kwenda kuzunguka na kutoa elimu ya kujihadhari na maambuzi ya virusi vya ugonjwa huo.

"Na kwa sasa hivi kwa sababu mnajua tupo kwenye kampeni kubwa ya kuzuia na kuelimisha wananchi kuhusu suala la ugonjwa wa corona, ambao sasa hivi limesababisha mpaka serikali imefunga baadhi ya taasisi na mikusanyiko mbalimbali,"alisisitiza Mkuu wa Wilaya.

Kwa mujibu wa Luhahula, kwa kuwa maofisa tarafa hao wamekabidhiwa vyombo vya usafiri wazitumie kuzunguka kwenye maeneo yao kuhakikisha agizo la kutoruhusu mikusanyiko inayotokana na pombe za asili linatekelezeka kwenye maeneo yao.


### NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **WAUNGWANA AUCTION MART, ADILI AUCTION COMPANY, JAGA AUCTION MART** na **RIMBO AUCTION MART** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba,Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | LUMUMBA | RIMBO ACTION MART | SHOO/M,FRANK | SHOO/M,FRANK | NYUMBA | TEGETA | 07/04/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 2 | LUMUMBA | JAGA ACTION MART | MWAKIMBWALA/ANTHONY, LUSEKELO | MWAKIMBWALA/ANTHONY, LUSEKEL0 | NYUMBA | MONGOLANDEGE | 07/04/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 3 | LUMUMBA | ADILI AUCTION MART | CHAKAPU/H,SAIDI | CHAKAPU/H,SAIDI | NYUMBA | ITALIAN-CHANIKA | 8/04/2020 SAA 08:00 ASUBUHI |
| 4 | PAMBA BRANCH | WAUNGWANA AUCTION MART | D4N - COMPANY - LIMITED | D4N - COMPANY - LIMITED | NYUMA-HOSPITAL NO.156 | KAHAMA | 08/04/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 5 | LUMUMBA | WAUNGWANA ACTION MART | NKWAMA/ZAKAYO,STEPHEN | NKWAMA/ZAKAYO,STEPHEN | KIWANJA | MBAGALA | 07/04/2020 ASUBUHI |
| 6 | TEMEKE | ADILI AUCTION COMPANY | KWANDE/J,PILI | KWANDE/J,PILI | NYUMBA | KISEMVULE | 9/04/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 7 | TEMEKE | ADILI AUCTION COMPANY | MTANDIKA/B,MWAHIJA | MTANDIKA/B,MWAHIJA | NYUMBA | MBAGARA KUU | 25/04/2020 SAA 4:00ASUBUH |
| 8 | TEMEKE | ADILI AUCTION COMPANY | MAKANDA/M,PETER | MWITA/KEMBAKI,ANSELMO | NYUMBA | VIKINDU - KAZOLE | 18/04/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474**
**JAGA AUCTION MART-0713123427**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215677902


## Majaliwa: Tutahakikisha corona haisambai zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Serikali inaendelea kufanya tathmini ili kuhakikisha inazuia ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19) isiweze kusambaa kwa kiasi kikubwa nchini.

Pia, Waziri Mkuu amevishukuru vyombo vya habari nchini kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Serikali katika kuelimisha umma namna ya kujikinga na virusi vya corona.

Waziri Mkuu alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Mawaziri na Makatibu Wakuu katika Kikao Kazi kilichofanyika kwenye ukumbi wa Hazina, jijini Dodoma.

Imeelezwa kuwa kinga dhidi ya virusi vya corona liwe ni jambo la kimkakati zaidi kuliko kusubiri kutibu, hivyo kwa sasa Serikali imeweka mkazo kwenye kuwahamasisha wananchi kujikinga na virusi hivyo.

"...Mawaziri hakikisheni katika kipindi hiki ziara za kwenda kukagua miradi zielekezwe kwa Wakurugenzi ikibidi kwa Makatibu Wakuu, Mawaziri mnatakiwa mjikite katika kukinga Taifa na corona."

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amesema Serikali imeunda kamati tatu kwa ajili ya kukabiliana na homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi ya corona (COVID-19). Kamati hizo ni ya Kitaifa ambayo itaongozwa na Waziri Mkuu na itahusisha baadhi ya Mawaziri, Makatibu Wakuu na Msemaji Mkuu wa Serikali.

## 14 wakiwamo wabunge watatu wa Chadema kizimbani

**Na Hellen Mwango**

WANACHAMA 14 wakiwamo wabunge watatu, meya, diwani na wengine tisa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka saba yakiwamo ya kudharau amri halali, shambulio, kuharibu mali na kutoa lugha ya kuudhi kwa jamii.

Washtakiwa hao ni Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalumu, Joyce Kishoa, Meya wa Ubungo, Boniface Jacobo na Diwani wa Segerea, Patrick Assenga.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Lenatus Mkude, Mkunde Mshanga na Wakili wa Serikali, Ester Martin, uliwataja washtakiwa wengine kuwa ni Henry Kilewo na Yohana Kaunya.

Wengine ni Kedmon Mhembo, Mshewa Karua, Khadija Mwago, Pendo Raphael, Cedilia Michael, Happy Abdallah na Stephen Kitomari.

Katika shtaka la kwanza, Mkude alidai kuwa Machi 13, mwaka huu katika Gereza la Segerea lililopo Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam washtakiwa wote 14 na wenzao ambao hawapo mahakamani, walikaidi amri halali ya Sajenti John, aliyekuwa na dhamana ya kulinda geti kuu la ngome ya gereza hilo ya kuwataka waondoke.

Mshanga alidai kuwa siku ya tukio la kwanza, washtakiwa wote 14 na wenzao ambao hawapo mahakamani, walifanya mkusanyiko isivyo halali katika Ngome ya Gereza la Segereana kutoa hofu, amani na utulivu kwa majirani.

Shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa siku ya tukio, katika Gereza la Segerea, washtakiwa wote 14 na wengine ambao hawapo mahakamani walishirikiana kufanya uharibifu wa geti kuu la gereza hilo mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania.

Pia, katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa siku ya tukio, Mdee alitamka lugha ya kuudhi ikiwamo kumkashifu Sajenti John wa Jeshi la Magereza huku akimwamuru kufungua geti hilo na kusababisha uvunjifu wa amani.

Vile vile, katika shtaka la tano, ilidaiwa kuwa siku na eneo la tukio mshtakiwa Bulaya alitamka maneno ya kuudhi mbele ya Sajenti John huku akimwamuru kufungua geti hilo na kusababisha uvunjifu wa amani.

Martin alidai katika shtaka la sita, siku na eneo la tukio, mshtakiwa Jacobo alitamka maneno ya kuudhi mbele ya Sajenti John akimwamuru kufungua geti hilo na kusababisha uvunjifu wa amani.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa shtaka la saba, siku na eneo la tukio, mshtakiwa Jacobo alimshambulia Sajenti John kwa kumvuta na kumchania shati la sare ya jeshi hilo akiwa anatelekeza majukumu yake kama mlinzi wa gereza hilo.

Washtakiwa wote walikana mashtaka yao.

Hakimu Shaidi alisema kila mshtakiwa atakuwa nje kwa dhamana kwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho na kitambulisho watakaotia saini ya hati ya dhamana ya Shilingi milioni nne.

Mkude alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika upande wa Jamhuri uliomba tarehe ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali pamoja na hati ya wito kwa washtakiwa 13 ambao hawapo mahakamani.

Washtakiwa wote walikamilisha masharti hayo kesi hiyo itasikilizwa maelezo ya awali Aprili 23, mwaka huu.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**DAVIDSON KABONDO LAZARUTIN**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **TVS STAR** yenye namba ya usajili **MC 223 CHR** Chassis namba **MD625AF74K1F03396** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **MAR/MUS/RB/240946/2020**

115677602

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**DONALD SEBASTIAN MAROGOTIN**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **TVS STAR** Yenye namba ya usajili **MC 546 CES** Chassis namba **MD625AF7XK1B00541** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **MAR/MUS/RB/240947/2020**

115677702

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SAFARI NJEMA TANZANIA LIMITED**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **TVS Star.** Yenye namba ya usajili **MC 237 CDH** Chassis namba **MD625AF49J1N00690** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **MAR/MUS/RB/240943/2020**

215677502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MJIBU RUFAA (MCA/84)**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**

**RUFAA MADAI NO. 06/2020**

**MDAI : JOHN LLEONARD**

**Anamdai**

**MDAIWA: JAFARI BUHAYE**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA RUFAA**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 17/04/2020 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshundwa .

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 20/3/2020.

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

..............................

**Hakimu Mkazi**

**Dodoma**

115677802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 47/2020**

**Ombi la NICOLAUS JULIAN Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JULIAN RASHID SELEMAN.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/02/2020

HAKIMU YA MWANZO MJINI MOROGORO

215677102

### KADI YA BAJAJI IMEPOTEA

**MWANAHAMISI ISSA KIBWANA** amepotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili MC 142 BTQ.Aina yake TVS KING,MG 86.Yenye chassis number: MD6M14PKXH4E78987 na Engine number: OK4EH4601176.Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi : **IRI/IRI/RB/218297/2020**

115677202


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BAYERN YAHOFIA KUMPOTEZA ALABA



**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich inahofia David Alaba anajaribu kulazimisha uhamisho wa kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid au Barcelona, kwa mujibu wa gazeti la BILD.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria, mkataba wake pale kwenye dimba la Allianz Arena unamalizika mwakani, na ameacha mlango wazi kuondoka.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wanajua kwamba, majaliwa ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 hayajulikani na wanahofia analazimisha kuondoka baada ya kumchukua wakala Pini Zahavi.

Zahavi mwenye umri wa miaka 76 pia ni wakala ambaye alichukuliwa na Robert Lewandowski mwaka 2018 wakati raia huyo wa Poland alipokuwa anataka kondoka Bayern kwenda Real Madrid.

Baada ya mazungumzo ya nguvu, mabosi wa Bayern walifanikiwa kumshawishi Lewandowski kuongeza mkataba wake wa kukaa pale Allianz Arena, lakini sasa klabu hiyo inakabiliwa tena na hali kama ile kwa nyota wao huyo.

Ripoti zaidi zinasema kwamba, baba mzazi wa Alaba, George yupo kwenye mazungumzo na Zahavi kuhusu kushirikiana, huku wawili hao wamejuana kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita baada ya kukutana nchini England.

Zahavi pia anajulikana ndiye aliyecheza dili la Neymar wakati anaondoka kule Barcelona kwa pauni 198 na kutua Paris Saint-Germain mwaka 2017.

# Smalling anataka kubaki Roma

**MILAN,** Italia

CHRIS Smalling atakuwa tayari kukatwa mshahara wake ili aweze kubakia AS Roma kwa mkataba wa kudumu, licha ya kutakiwa na Arsenal.

Beki huyo Mwingereza amekuwa nguzo muhimu ya safu ya ulinzi tangu alipojiunga na miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa mkopo kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Muda wake wa kukaa pale kwenye uwanja wa Olimpico unatarajiwa kufikia mwisho Juni mwaka huu, ingawa Sky Sports Italia imeripoti kwamba, Smalling anataka kuongeza muda wa kukaa na klabu hiyo.

Imeripotiwa kwamba, mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 30 amefurahia muda wake wa kukaa pale Roma na sasa yupo tayari kupunguziwa mshahara wake ili kuendelea kubakia klabuni hapo.

Manchester United imeripotiwa kwamba, inataka pauni milioni 32 ili kumwachia mchezaji huyo.

Wakati huo huo, Arsenal, ambayo inakabiliwa na matatizo kwenye safu yake ya ulinzi, imeonyesha nia ya kutaka kumsajili Smalling.

Mlinzi huyo wa kati alijiunga na Mashetani Wekundu karibia miaka 10 iliyopita kipindi cha majira ya joto mwaka 2010.







# Dejan azigonganisha Lazio, Arsenal na Spurs

**LONDON,** England

KLABU ya Lazio imejiunga kwenye mbio moja za kuwania kumsajili mlinzi wa kati wa Liverpool, Dejan Lovren ambaye anaonekana hayupo tayari kuongeza mkataba wake wa sasa unaomalizika Juni 2021.

Miamba hao wa Ligi Kuu England, Arsenal na Tottenham pia zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi huyo wa Croatia, ambaye amekosa namba pale Anfield.

Lazio awali walimtaka Lovren wakati wa dirisha la usajili la Januari, lakini hawakuweza kufikia bei waliyoitaka Liverpool ya pauni milioni 20.

Kwa mujibu wa La Gazzetta dello Sport, bei ya Lovren imeshuka kutokana na kutokuwa kwenye kiwango katika kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ameripotiwa kwamba, yupo tayari kutafuta changamoto mpya kabla ya kustaafu soka, lakini hajaonyesha ishara wapi anataka kwenda.

# Nyota Barca wakubali kukatwa mishahara

**BARCELONA,** Hispania

WACHEZAJI wa Barcelona wapo tayari kukatwa mishahara yao kama wakiombwa kufanya hivyo, wakati klabu hiyo ikikabiliwa na matatizo ya kifedha kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kwa mujibu wa gazeti la AS, 'hawataweka kipingamizi' baada ya mazungumzo kati ya maofisa wa timu na Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu.

Wakurugenzi walitangaza Septemba kwamba, ungekuwa msimu wao wa kwanza kuvunja rekodi ya kuingiza mapato ya euro bilioni moja msimu huu, lakini ilitegemea zaidi kuuza wachezaji ambao wangeingiza pauni milioni 92.

Lakini kutokana na kusimamishwa kwa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, mapato ya Barcelona yameathirika.

Klabu hiyo ilikuwa ikitegemea kuingiza fedha kwa mauzo ya tiketi, watalii wanaotembelea makumbusho yao pamoja na mauzo ya jezi, lakini yote yameathirka na kusimamishwa kwa ligi hiyo na kuna uwezekano baadhi ya wafadhili kutotoa fedha.

Klabu hiyo imesema kusimamishwa tu kwa mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli peke yake kumewagharimu pauni milioni 5.5.

Msimu uliopita makumbusho yao yaliingiza kiasi cha pauni milioni 55 kwa kutembelewa na wageni.




# RIO: WAN-BISSAKA NI BEKI BORA




**MANCHESTER,** England

RIO Ferdinand amesisitiza kuwa, Trent Alexander-Arnold na Aaron Wan-Bissaka watakuwa 'mashine' kwenye nafasi ya beki wa kulia, huku akidai kwamba, nyota wa Mashetani Wekundu ni bora zaidi kwenye mbinu za ulinzi kuliko mwenzake wa Liverpool.

Wan-Bissaka amekuwa na mwanzo mzuri pale Manchester United tangu alipotua kwa ada ya pauni milioni 50 akitokea Crystal Palace kipindi cha majira ya joto, huku Alexander-Arnold akiendelea kuonyesha uimara kwake kwa vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool.

Alexander-Arnold anachukuliwa kama ndie beki bora zaidi wa kulia wa England huku akiwa amecheza mechi nyingi kwenye timu ya taifa, lakini Ferdinand anaamini Wan-Bissaka anaweza kupambana na kumzidi nyota wa Liverpool na kuwa chaguo la kwanza kwa kocha, Gareth Southgate.

"Kama ukiwaangalia kwa makini kwa mbinu zao za uchezaji uwanjani kwa pamoja kati ya Aaron Wan-Bissaka na Trent Alexander-Arnold, utampata mmoja kuwa bora zaidi," alisema Ferdinand wakati wa mahojiano yake kwenye mtandao wa Instagram.

"Aaron Wan-Bissaka akicheza mmoja dhidi ya mmoja ni bora sana, nimemwona (Raheem) Sterling akicheza dhidi yake. Sterling alikuwa na wakati mgumu kumpita Wan-Bissaka.

"Alexander-Arnold kimbinu ya ukabaji bado hajamfikia Wan-Bissaka na nina amini watakuwa na ushindani mkali zaidi kwa siku zijazo."

Wan-Bissaka bado anapigania kupata nafasi ya kuitwa katika kikosi cha England chini ya England, huku Alexander-Arnold na Kieran Trippier wakiwa ndio chaguo la kwanza dhidi yake.

# *Juventus kumwongezea mkataba Buffon*

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imeripotiwa kwamba imefikia makubaliano na Gianluigi Buffon, Giorgio Chiellini na Blaise Matuidi kwa ajili ya kuongeza mikataba yao.

Wachezaji hao mikataba yao ya sasa inamalizika Juni 30, mwaka huu lakini kwa mujibu wa ripoti ya Goal, wamepanga kubakia Juventus kwa ajili ya msimu ujao, ingawa bado hawajatia saini mikataba hiyo mipya.

Golikipa mkongwe Buffon amecheza mechi 11 tu kwa Juventus msimu huu tangu aliporudi klabuni hapo akitokea Paris Saint-Germain.

Licha ya umri wake wa miaka 42, Buffon bado haonyeshi nia ya kutaka kustaafu kucheza soka.

Beki wa kati, Chiellini pia anataka kubakia klabuni hapo, ambako amecheza tangu mwaka 2005.

Msimu huu Chiellini amecheza mechi tatu tu kutokana na kukabiliwa na majeruhi ya mara kwa mara, lakini hivi karibuni amerudi dimbani.

Wakati huo huo, Matuidi ambaye amekuwa hapo Juventus tangu 2017, msimu huu kiungo huyo amecheza mechi 31.

Matuidi, pamoja na mchezaji mwenzake wa Juventus, Daniele Rugani, walipatikana na virusi vya corona.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA KUMWEKA SOKONI GRIEZMANN

Ni kutokana na kiwango alichokionyesha Mfaransa huyo tangu alivyotua klabuni hapo...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inampango kumweka sokoni Antoine Griezmann baada ya kukaa klabuni hapo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja, kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania.

**Mfaransa huyo alijiunga na miamba hao wa Katalunya akitokea Atletico Madrid kwa ada ya pauni milioni 108 ambayo ilikuwa kwenye kipengele cha kuuzwa kwenye mkataba wake.**

Lakini Griezmann kiwango chake chini ya kikosi hicho cha kocha, Quique Setien hakijawa kama kilivyotarajiwa, akifunga mabao 14 tu katika mechi 37 msimu huu.

Na gazeti la Diario Sport limedai Barcelona sasa wapo tayari kusikiliza ofa ya zaidi ya pauni milioni 92 kwa Mfaransa huyo ili kuwekeza kwa wachezaji wengine nyota.

Klabu hiyo ina matumaini ya kukifumua kikosi hicho kipindi cha majira ya joto licha ya mlipuko wa virusi vya corona, lakini watahitaji kwanza kununua wachezaj wa kikosi cha kwanza kama mipango yao ya kuwanunua Neymar kutoka Paris Saint-Germain na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez haitafanikiwa.

Na ripoti zinadai kwamba, Griezmann atatazamiwa kuwaniwa na klabu za PSG, Manchester United na Chelsea.

Habari hizi zimekuja baada ya gazeti la Daily Mail kubainisha Jumamosi kwamba, klabu hiyo inahitaji wachezaji wao wanaingiza kitita kikubwa cha fedha kukatwa mishahara yao ili kukabiliana na matatizo ya kifedha yanayoitikisa klabu hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Ni Lionel Messi pekee ambaye analipwa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki amemzidi Griezmann ambaye analipwa mshahara wa pauni

## ZISIKUPITE

### BABA AMMALIZA JOVIC

BABA mzazi wa mchezaji wa Real Madrid, Luka Jovic, 22, amesema mtoto wake inabidi akubali adhabu yoyote - hata kufungwa jela endapo atakutwa na hatia ya kukiuka masharti ya karantini kwa kusafiri kwenda kumtembelea mpenzi wake jijini Belgrade. ***(Marca)***

### BARCA YAMWANIA LAPORTE

KLABU ya Barcelona wana nia ya kumsajili beki wa Manchester City na Ufaransa, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 25, wakati wa kipindi cha majira ya joto. ***(Mundo Deportivo)***

### SKRINIAR AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Paris St-Germain, Real Madrid na Manchester City zote zinawania saini ya beki wa Inter Milan na timu ya taifa ya Slovakia, Milan Skriniar, 25. ***(Calciomercato)***

### KOULIBALY KUONDOKA NAPOLI

BEKI Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 28, yupo tayari kuihama klabu ya Napoli mwishoni mwa msimu, huku Manchester United ikihusishwa na kutaka kumsajili beki huyo wa kati wa Senegal. ***(Mirror)***

### ARSENAL, LIVERPOOL VITANI

KLABU za Liverpool na Arsenal zimeripotiwa kufuatilia maendeleo ya beki wa klabu ya Eintracht Frankfurt ya Ujerumani, Evan Ndicka mwenye umri wa miaka 20, kabla ya msimu kusimamishwa. ***(Sky Sports)***

### ARSENAL YAPANGA KUJIFUA

KLABU ya Arsenal ipo katika mazungumzo na madaktari wa klabu nyingine za EPL juu ya uwezekano wa wachezaji wake kuanza mazoezi wiki hii. ***(Daily Mail)***

### HIGUAIN AVUNJA MASHARTI

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Gonzalo Higuain mwenye umri wa miaka 32, amevunja masharti ya Karantini nchini Italia na kusafiri mpaka Argentina kwenda kumuuguza mama yake ambaye anaumwa saratani. ***(Sun)***

### BARCA KUPUNGUZA MISHAHARA

BARCELONA wapo katika mazungumzo na wachezaji wao nyota ili kupunguza mishahara yao kutokana na klabu hiyo kuona kuwa haitaweza kuhimili bajeti ya mishahara inayofikia euro bilioni moja kwa kipindi cha msimu kilichobakia. ***(Marca)***

### BELARUS YAMSHANGAZA HLEB

KIUNGO wa zamani wa Arsenal na Barcelona, Alexander Hleb amedai "hakuna mtu anayejali" kuhusu virusi vya corona nchini mwake Belarus, nchi pekee ambayo bado inaendelea na Ligi Kuu kwa sasa. ***(Sun)***

### DORTMUND YAIFUNIKA UNITED

MANCHESTER United inatajwa kumpa ofa ndogo ya mshahara nyota, Jude Bellingham ukilinganisha na aliyopewa na Borussia Dortmund, vigogo hao wa Ujerumani wanajipanga kumsajili mchezaji huyo ili kuzipa nafasi itakayoachwa na Jadon Sancho. ***(Mail)***

### MANCHESTER UTD YAKUBALI

BOSI wa Manchester United, Ed Woodward anasisitiza kuwa hawezi kubadilisha mawazo au kupinga nafasi ambayo Liverpool wanayo katika mbio za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England. ***(Mail)***

## Gwambina kusajili nyota Simba, Yanga

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwa na asilimia zaidi ya 90 ya kupanda daraja, uongozi wa Gwambina FC umesema umeanza kuandaa bajeti kwa ajili ya mchakato wa usajili wa wachezaji watakaowatumia katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Gwambina FC, Daniel Donald, alisema wamejipanga vema kuandaa 'kitita' cha fedha ili kusajili wachezaji watakaosaidia kikosi chao kufanya vizuri na kuonyesha ushindani katika msimu ujao.

Donald alisema mikakati yao ni kukiboresha kikosi chao kwa lengo la kuwa moja ya timu zenye ushindani na si kuzindikiza wengine.

"Tumejipanga kusajili wachezaji wazuri, lakini tuweke wazi pia tutaangalia nyota watakaoachwa Simba, Yanga na Azam FC, tunajua kwetu watatusaidia kutokana na uzoefu," alisema Donald.

Aliongeza sema mipango yao ni kuona timu yao inaingia katika Ligi Kuu na kuleta ushindani, imewalazimu kutenga bajeti ya maana kwa ajili ya kuboresha kikosi chao kusajili nyota wazuri wa kigeni na hata kuangalia wanaoachwa na timu kubwa hapa nchini.

Gwambina yenye pointi 40, inaongoza katika msimamo wa Kundi B kwenye Ligi Daraja la Kwanza.

## Polisi Tanzania kurejea kambini

**Na Shufaa Lyimo**

ILI kujiweka imara kwa ajili ya kumalizia msimu wa 2019/20 wa Ligi Kuu Bara, uongozi wa Polisi Tanzania umesema kikosi chake kitaingia kambini Machi 30, mwaka huu.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hamsini Malale alisema wameamua kuanza kambi mapema ili kuwaweka sawa wachezaji wao, huku wakisubiri tarehe mpya ya kuendelea kwa ligi hiyo.

Kocha huyo alisema maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), yamemwalibia mipango yake katika kukijenga kikosi chake kuelekea mechi za hatua ya lala salama.

"Niliwapa wachezaji wangu mapumziko ya siku 10, baada ya kupata taarifa ya kusimamishwa kwa Ligi Kuu kutokana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, kwa upande wetu naona corona imetuathiri kwa kiasi kikubwa, nilikuwa tayari nimewapanga na kuwaandaa wachezaji wangu na mchezo uliokuwa mbele yetu, lakini haukuchezwa tena, inapidi tuanze upya," alisema Malale.

Aliongeza baada ya wachezaji kurejea, wote watafanyiwa vipimo kabla ya kuanza kwa mazoezi ya pamoja ili kujua hali zao za kiafya kwa wakati huo.

# YANGA YAFUNGUKA ILIVYOIZIDI SIMBA KUMTULIZA TSHISHIMBI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kumshawishi kiungo wake wa kimataifa Papy Tshishimbi kubakia klabuni kwake, uongozi wa Yanga umesema ulifahamu mipango waliyokuwa nayo wapinzani wao, Simba katika kumwinda Mkongomani huyo, imeelezwa.

**Tayati Yanga na Tshishimbi wamefikia katika hatua nzuri ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo.**

Tshishimbi ni miongoni mwa wachezaji wa Yanga ambao mikataba yao inakaribia kumalizika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema wamefikia katika hatua nzuri na kiungo huyo ambaye ni mmoja wa wachezaji ambao wamependekezwa na Kocha Luc Eymeal kubakia klabuni hapo.

Mwakalebela alisema kuwa uongozi wa klabu hiyo utaendelea na mchakato wa kuwapa mikataba mipya nyota wote ambao wameonyesha kiwango kizuri na benchi la ufundi linahitaji kuendelea kufanya nao kazi katika msimu ujao.

"Baada ya kufanikisha kwa Bernard Morrison, sasa tunaendelea na mchakato wetu wa kuzungumza na wachezaji wengine ambao mikataba yao ipo ukingoni, tayari tumeshakutana na Tshishimbi kwa ajili kumwongezea mkataba mpya wa kuitumikia timu yetu," alisema Mwakalebela.

Aliongeza kuwa wanaamini usajili watakaofanya sasa utalenga kutimiza mipango ya kufanya vizuri katika msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano yote watakayoshiriki ndani na nje ya nchi.

"Tunachokifanya ni kuendelea kukijenga kikosi chetu, tunataka kuwa na timu bora zaidi ya sasa, timu itakayokuwa inatupa matokeo chanya katika kila mechi, Mwakalebela alisema.

Aliongeza kikosi chao kimekuwa na mabadiliko tangu ujio wa Mbelgiji Eymael na wanaamini kitaendelea kuwa imara na kufanya vema katika michezo iliyosalia ya Ligi Kuu Bara na mashindano ya Kombe la FA.



Wachezaji wa timu ya Sunderland wakifanya mazoezi ili kuimarisha viwango vyao katika viwanja vya Jakaya Kikwete (JKM Park), jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Parimatch yaendelea kumwaga mamilioni*

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kuahirishwa kwa mechi nyingi barani Ulaya na hata hapa nchini kwa kipindi cha siku 30 kutokana na hofu ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19), Kampuni ya michezo ya kubahatisha Parimatch imeendelea kutoa mkwanja mnono pamoja na bonasi kabambe kwa wateja wake wanaobashiri na kushinda michezo ya Virtual games.

Hata hivyo Parimatch inawakumbusha wateja wake kuzingatia na kufuata maelekezo yanayotolewa na mamlaka husika juu ya kujikinga na virusi vya ugonjwa huo wa corona.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Masoko wa Parimatch Tanzania, John Mwakalonge, alisema kampuni yao imejipanga vizuri katika kutoa huduma bora na za kisasa kwa kupitia tovuti yao www.parimatch.co.tz kwa lengo la kuendelea kuwapa fursa ya kubashiri wateja wao pindi ligi nyingine zimesimama au zitakapokuwa zimemaliza msimu wake.

"Parimatch tuna wigo mpana wa michezo inayowawezesha wateja wetu kushinda na kupata pesa kutokana na ubashiri. Ni kweli kuwa ligi nyingi zimeahirishwa kwa sasa ulimwenguni kote, lakini kwa upande wetu tuna virtual games ambayo inajumuisha michezo yote ambayo watu walikuwa wakicheza," alisema Mwakalonge.

Aliongeza katika kipindi hiki pia Parimatch imeweza kutoa fursa ya kipekee ya uwakala kwa wateja wake wote walio ndani ya Tanzania kwa kugawana asilimia 25 ya faida inayopatikana kutoka kwa wateja wapya waliounganishwa na mawakala hao.

"Parimatch tumeamua kutoa fursa kwa Watanzania, kwa kutengeneza pesa kiurahisi katika muda wao wa ziada. Njooni huku mjitajirishe Watanzania wenzangu, mshike mkono rafiki yako ili mtoke kimaisha kwa pamoja," alisema Mwakalonge.

Alisema wanajivunia kuanzisha vitu vipya na vya kisasa vinavyoendana na teknolojia, jambo ambalo linasaidia kuchangamsha soko la michezo ya kubahatisha na kuwapa fursa watumiaji wake katika kubashiri mechi katika wigo mpana.

Kiongozi huyo alisema pia tangu Parimatch ilipoingia sokoni imeweza kubadilisha hali ya soko ya zamani kwa kutoka kwenye kamari hadi kuwa burudani, hali ambayo imevutia mashabiki wengi.

# Michezo

Jumanne Machi 24, 2020
Nipashe



Barca kumweka sokoni Griezmann UKURASA 30



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (kushoto), akijaribu kumtoka beki wa Yanga, Lamine Moro katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa Machi 8, mwaka huu. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MAKTABA**

# NDEMLA AZITESA SIMBA, YANGA

## ●●● Ni baada ya kiungo huyo kukataa kusaini mkataba mpya, safari yake ya kucheza soka Sweden sasa...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukosa namba katika kikosi cha kwanza cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba, Said Ndemla (pichani) amekataa kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo na kuelekea Sweden kucheza soka la kulipwa, imefahamika.

**Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema Ndemla ambaye mkataba wake na vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu, amewakatalia mabosi wake wa Simba kusaini mkataba ili kukamilisha mchakato wake wa kwenda kujiunga na klabu ya AFC Eskilstuna ya nchini humo.**

Chanzo chetu kilisema kuwa Ndemla alifaulu katika majaribio lakini klabu hiyo ilikuwa tayari kumsajili akiwa ni mchezaji huru.

"Baada ya kuona nafasi ya kucheza ni ndogo na siku zinakwenda, Ndemla hakukubali kusaini, ameshawishiwa mara kadhaa kusaini, lakini amewakatalia viongozi, kubwa ni kutokana na kuwa na ahadi ya kusajiliwa Sweden, lakini kwa sharti la kuwa mchezaji huru," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza AFC Eskilstuma bado inamhitaji Ndemla baada ya miaka miwili iliyopita kushindwa kumsajili kutokana na dau la juu walilotakiwa kulipa ili kuvunja mkataba wake na Wekundu hao wa Msimbazi.

"Mkataba wa Ndemla upo ukingoni, hivyo hii ni nafasi ya kiungo huyo kwenda kucheza soka la kulipwa nchini humo kulingana na uongozi wa timu hiyo kumhitaji



akiwa mchezaji huru," alisema chanzo hicho. Taarifa nyingine zinasema kuwa Yanga pia imetajwa kumwania kiungo huyo aliyepandishwa akitokea Simba B, lakini amekataa kutua Jangwani.

Kiongozi mmoja wa juu wa Yanga aliliambia gazeti hili kuwa wamefanya mawasiliano na kiungo huyo kwa nyakati tofauti, lakini aliendelea kushikilia msimamo wake wa kutosaini mkataba.

"Tuliona hii nafasi nzuri kwetu kumpata Ndemla kwani hapati nafasi katika kikosi cha kwanza, lakini tumeshindwa baada ya kutueleza kwamba mipango yake kwa sasa ni kucheza soka la kulipwa, hivyo huenda akaondoka baada ya msimu huu kumalizika, kwa sababu alifuzu majaribio," alisema kiongozi huyo.

Klabu za Ligi Kuu nchini zimeonekana kutumia muda huu wa mapumziko kuanza mchakato wa usajili kwa lengo la kulinda nyota wake inaowahitaji.

# Morrison: Mengi mazuri yanakuja

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa Yanga ambaye kwa sasa ameiteka mioyo ya mashabiki na wanachama wa klabu hiyo, Bernard Morrison, amesema anafurahi kuona 'amekubalika' mapema ndani ya klabu hiyo na hali hiyo inampa nguvu ya kujipanga kufanya makubwa zaidi.

Morrison alisema ili kufikia malengo ya timu hiyo, wachezaji wanahitaji kupambana kuhakikisha wanashinda mechi zao za ligi zilizobakia na mashindano ya Kombe la FA.

Mshambuliaji huyo alisema kuwa 'mapenzi' wanayopata wachezaji wa timu hiyo kutoka kwa mashabiki wa Yanga ni sababu inayowafanya wajitume katika kila mechi wanayocheza na kusahau changamoto zinazowakabili.

"Ningependa kuwashukuru mashabiki kwa kunikubali, nimekuwa na wakati mzuri, nimekuwa nikipata zawadi mbalimbali kutokana na uchezaji wangu, hii inanifanya nijipange zaidi kuisaidia timu yangu, nimejifunza vitu vingi nilipokuwa Orlando Pirates," alisema Morrison.

Hata hivyo alisema ili kumaliza katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi, wanatakiwa kufunga mabao zaidi na hatimaye kujihakikishia nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa na kuwapa furaha mashabiki wao.

"Ninaheshimu ajira yangu ndani ya Yanga, nitaitumikia kwa nidhamu, mipango yangu ni kutimiza malengo yangu, lakini huu ni mpira, kwa sasa naomba nieleweke nguvu na akili zangu nazielekeze kuisaidia Yanga na si timu nyingine," Morrison aliongeza.

Ili kuhakikisha inaendelea kummiliki Mghana huyo, Yanga imempa mkataba mpya wa miaka miwili ambao utamalizika Juni, 2022 na uamuzi huo ulimaliza tetesi za kujiunga na Simba.

Mshambuliaji huyo aliifungia Yanga bao pekee katika mechi dhidi ya watani zao Simba, ushindi ambao unaendelea kuwapa faraja wanachama wa klabu hiyo ambao baadhi wamekata tamaa ya kutwaa taji la Ligi Kuu Bara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >